
SUPA JACKPOT
TZS.1,072,549,524
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**IHC** yawekeza Bil. 940/- kwenye kampuni ya Adani


Nipashe TESA
Jumanne Januari 31, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Mamia walivyonusuriwa na ujinga, umaskini hata njaa
Ndivyo shule inavyoandaa wasomi jasiri, waibua fursa, wanaong'ara
ELIMU
NA SABATO KASIKA
Bunge linaposhangazwa, kuhoji kozi Chuo Nyerere
•Ni udahili wa walimu wakati maelfu ni 'jobless' mitaani

UKURASA 11

Nipashe
Jumanne Januari 31, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581207
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# HALI MBAYA

## MASOMO ya ufundi ufaulu wa kuchechemea, wadau elimu watoa angalizo...

*Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Remy Ngoy Lumbu (wa nne kushoto) pamoja na Mratibu wa Kimataifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Onesmo Olengurumwa (wa pili kushoto), Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Tume hiyo iko nchini kwa mwaliko wa serikali kufuatia ombi lililotolewa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu. **PICHA: IKULU**

## Samia: Haya hapa maeneo makuu yatakayoibeba nchi kwa kilimo

UKURASA 3

## Wagonjwa akili waongezeka mara tano Mloganzila

UKURASA 4

**MICHEZO** MANGUNGU: SASA KAZI NI MOJA TU SIMBA SC UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Hali mbaya matokeo ya shule za ufundi

**Na Restuta James**

WAKATI asilimia 79.92 ya watahiniwa wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka jana wamefeli somo la Hisabati, Nipashe imebaini hali mbaya ya ufaulu kwa shule mahususi kwa ufundi.

Matokeo hayo yaliyotangazwa juzi na Baraza la Mitihani (NECTA), yanaonyesha shule za ufundi zinazomilikiwa na serikali, zimefanya vibaya kwenye masomo ya ufundi.

Mathalani, Shule ya Ufundi Iyunga iliyoko mkoani Mbeya imepata wastani wa jumla wa daraja B, lakini matokeo ni mabaya kwenye masomo ya ufundi.

Wastani wa jumla wa masomo ya Uhandisi wa Sayansi, Ujenzi wa Majengo, Uchoraji wa Usanifu, Useremala, Uchoraji na Uandishi Mabango, wahitimu wamepata daraja D.

Vilevile, wastani wa jumla wa masomo ya Uashi na Ufundi Matofali, Mabomba, Ufungaji wa Umeme, Sayansi ya Uhandisi wa Umeme, Huduma za Redio na Televisheni pamoja na Uchoraji wa Umeme ni C.

Hata hivyo, kuna wanafunzi wachache ambao katika baadhi ya masomo hayo wamefaulu kwa daraja la A.

Kwa Sekondari ya Ufundi Moshi, wastani wa jumla wa masomo manne ya Sayansi ya Uhandisi, Ujenzi wa Majengo, Uchoraji wa Usanifu na Huduma za Redio na Televisheni ni D huku ikipata wastani wa C kwenye masomo ya Ufundi Matofali na Uashi, Sayansi ya Uhandisi wa Umeme na lile la Ufungaji wa Umeme.

Shule hii imefanya vizuri kwenye somo la Uchoraji wa Umeme kwa kupata wastani wa B na wastani wa C kwenye Hisabati.

Sekondari ya Ufundi Tanga ina wastani wa jumla wa D katika masomo matano ya ufundi ya Uhandisi wa Kisayansi, Ujenzi wa Majengo, Uchoraji wa Usanifu, Utengenezaji wa Mitambo na Vifaa na Uchoraji wa Mitambo.

Wastani wa jumla wa Sekondari ya Ufundi Mtwara kwa masomo yote ni daraja C wakati masomo matano ya ufundi ina wastani wa jumla wa daraja D.

Kwa Sekondari ya Ifunda, wastani wa jumla wa shule ni daraja B lakini masomo matatu ya ufundi imepata wastani wa D na imefanya vizuri kwenye masomo 10 ya ufundi ambayo imepata wastani wa C.

Shule hiyo pia imepata wastani wa B kwenye masomo mawili ya ufundi ambayo ni Uhandisi wa Sayansi ya Umeme na Uchomeleaji na Utengenezaji wa Vyuma huku ikiwa na wastani wa jumla wa B kwenye somo la Hisabati.

Sekondari ya Ufundi Musoma ina wastani wa jumla wa daraja B na wanafunzi wamefaulu vizuri masomo ya sanaa, biashara na sayansi.

Ufaulu wa jumla kwenye masomo matatu ya ufundi ni daraja C na somo la Sayansi ya Uhandisi Umeme pamoja na Hisabati ina wastani wa daraja B.

**WADAU WANENA**

Mtaalamu wa Uchumi aliyewahi kufundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Donath Olomi, akitoa maoni yake kwa Nipashe jana kuhusu matokeo hayo, alisema kuna vikwazo vingi kwenye shule za umma, hususani za ufundi, vinavyojumuisha uhaba mkubwa wa walimu na vifaa vya kufundishia.

"Walimu na vifaa vya kufundishia katika masomo ya sayansi ni shida kubwa kweli. Na hilo tatizo limeanzia kwamba hata ufaulu wa watu wanaopaswa kwenda kusomea ualimu umekuwa ni mdogo," alisema.

Aliongeza kuwa licha ya uhaba wa walimu, mtaani kuna walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati ambao hawajaajiriwa.

"Serikali haijaajiri muda mrefu, kwa hiyo kumetokea pengo kubwa sana la walimu na hilo pengo ni kubwa zaidi kwa walimu wa sayansi... kwanza hili pengo lizibwe haraka iwezekanavyo na kuwe na juhudi maalum za kukabiliana na uhaba huu," alishauri Dk. Olomi.

Alisema tatizo lililoko kwenye shule za ufundi linakwenda hadi kwenye vyuo vya masomo hayo, akieleza kwamba ni kawaida kukuta havina vifaa muhimu vya ufundishaji, jambo linalowakwamisha wahitimu kwenye soko la ajira.

Mdau wa elimu jijini Dar es Salaam, Amina Swalehe, aliiambia Nipashe jana kwamba vyuo vingi vya serikali vilivyojengwa miaka ya 1960 vinaendelea kuwafundisha wanafunzi kwa kutumia mitambo na vifaa vya zamani.

"Unaweza kuona maendeleo ya teknolojia duniani na jinsi inavyobadilika lakini serikali haiwekezi vifaa kwenye vyuo au shule za ufundi... hili linapaswa kutazamwa upya haraka iwezekanavyo," alitoa hadhari.

Rais mstaafu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Gratian Mukoba, akizungumza na Nipashe jana kuhusu matokeo hayo, alisema serikali inapaswa kuongeza nguvu kwenye sekta ya elimu kwa kuwa matokeo ya mitihani yanatoa picha ya hali halisi.

"Kuna kitu kinapungua ambacho mimi sikijui... walioko kwenye mfumo (wa elimu) wafanye utafiti na wakitatue ili kuokoa elimu yetu," alishauri.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Sylvia Lupembe, aliiambia Nipashe jana kuwa wizara inafanya uchambuzi wa matokeo yote kwa ujumla na itatoa taarifa baadaye.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
30/01/2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO** tarehe **01/02/2023** kampuni ya **ICHEETAH LOGTECH TANZANIA LTD** itasafirisha malori yenye vipimo vikubwa kutoka Dar es Salaam kuelekeaa Tunduma malori hayo yenye namba za usajili:

**T505DZD/T904DZE na T163EAF/T624EAJ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**I. T505DZD/T904DZE Urefu-18m Upana -5.5m ,Kimo-4.8m**
**II. T163EAF/T624EAF Urefu-18m Upana -4.9m ,Kimo-4.8m**

3. Njia itakayotumika: Dar es Salaam hadi Tunduma Kupitia Iringa gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
30/01/2023

JUMATANO

TAARIFA KWA UMMA

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO** tarehe **01/02/2023** kampuni ya **AFRICA WAKAWAKA LOGISTICS CO. LTD** itasafirisha mzigo mkubwa kutoka Dar es Salaam kuelekeaa Tunduma kupitia Mikumi.

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**1. T363 DYM / T 533 DXY**
**2. T 855 EBJ/ T606 EBM**

VIPIMO
**Urefu - 22m Upana - 4.7m, Kimo - 5.0**

Gari litasafiri mzigo kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

# Serikali: Bei za vyakula zitashuka

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imewatoa hofu Watanzania na kuwataka kuwa wavumilivu kuhusu kupanda kwa bei ya vyakula, ikieleza kwamba hali iliyopo sasa ni ya mpito na bei itashuka.

Imesema imeshaweka mikakati ya kuhakikisha hali iliyopo sasa inaondoka na taifa halitarudi tena katika nyakati kama hizi.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan jijini Dakar, Senegal Januari 25 hadi 27 mwaka huu.

"Mimi ninaamini hii ni transition (mpito) na bei ya chakula itashuka. Tutaondoka kwenye taifa la kuwa tegemezi, kwamba kwa miaka minne ijayo taifa litakuwa katika nafasi nzuri.

"Ni ukweli bei ya vyakula imepanda lakini ni vizuri tukafahamu kwanza serikali hii iliingia madarakani ilikutana na matatizo makubwa manne, la kwanza ni ugonjwa wa corona, ambao uliathiri nchi katika usambazaji wa pembejeo, kwa maana ya kusafirisha nje na kuleta ndani.

"Pili, ni vita vya Ukraine na Russia, tatu ni mabadiliko ya tabianchi na nne ni kupanda kwa gharama za mafuta duniani," alifafanua Bashe.

Alisema matatizo hayo ikiwamo vita vya Ukraine na Russia yameiathiri nchi kwa sababu Tanzania ni waagizaji wa bidhaa za kilimo, mbegu na mbolea kutoka nje.

Alifafanua kwamba chakula kinachotumika leo hakijazalishwa sasa bali kilizalishwa msimu wa mwaka 2021/22.

Alisema bei ya mbolea kwa mwaka 2020/21 ilikuwa ni wastani wa Dola za Marekani 300, lakini ulipoingia msimu wa kilimo wa mwaka 2021/22 ambao mavuno yake yalifanyika Juni mwaka jana, bei ya mbolea ilipanda kwa zaidi ya asilimia 200.

Bashe alisema mkulima aliyelima mpunga wilayani Mbarali mkoani Mbeya, mfuko wa mbolea ya kupandia ulipanda kutoka Sh. 50,000 hadi 140,000, mfuko wa mbolea ya kukuzia ulipanda kutoka Sh. 45,000 hadi 120,000, hivyo kusababisha gharama za uzalishaji kwa mkulima kuongezeka.

"Leo ukinunua mchele daraja la kwanza wilayani Nzega, ukienda mashineni utaununua kwa Sh. 2,500, hadi Sh. 2,700, ukiusafirisha kuja Dar es Salaam mwaka 2020 gharama ya kusafirisha kwa kilo moja ilikuwa Sh. 70, leo ni Sh. 210

"Hapo maana yake gharama ya mafuta imepanda, gharama za usafirishaji zimepanda. Sasa huyu mkulima wa Mbarali gharama za uzalishaji mwaka 2020 na msimu wa kilimo wa mwaka 2021/22 zilipanda kwa zaidi ya asilimia 200, sasa ni lazima gharama za chakula zitapanda," alisema Bashe.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

Bashe alisema Rais Samia alipoingia madarakani aliweka ruzuku katika mafuta, mbolea na mbegu.

Alisema: "Hali hiyo inamaanisha kwamba mkulima aliyenunua mbolea katika msimu wa mwaka 2021/22 kwenda shambani kuzalisha, aliyenunua kwa Sh. 140,000 kwa mfuko mmoja. Msimu wa kilimo 2022/23 ambao chakula chake tutakivuna kuanzia Aprili, Mei na Juni mkulima huyu alinunua mfuko wa mbolea kwa Sh. 70,000."

Alisema hatua ya pili, serikali imeweka mikakati ya muda mrefu ili tatizo lililotokea lisijirudie tena.

Bashe alisema Rais Samia anatarajia kuzindua kiwanda cha mbolea kitachozalisha metric tani milioni moja, wakati mahitaji ya mbolea kwa sasa nchini ni tani 400,000 hadi 600,000.

Alitaja mkakati mwingine ni serikali kuanza kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji na kuachana na kutegemea mvua, kwamba mabonde 22 yapo katika utafiti wa kuhakikisha maji yake yanatumika katika kilimo cha umwagiliaji na serikali imetenga Sh. bilioni 36 katika mchakato huo.

**WANUNUZI KUTOKA NJE**

Bashe pia alitoa ufafanuzi kuhusu wafanyabiashara kutoka nje kuja nchini na kununua mazao, akisema: "Mazao ya kilimo ni ya mkulima, ni mali yake na sio ya umma, wana haki ya kuyauza popote na kumuuzia mtu yeyote. Tutamruhusu mtu yeyote kutoka sehemu yoyote kwenda kununua mazao sehemu yoyote".

Bashe alisema endapo serikali ikihitaji kununua mazao itakwenda kununua kwa wakulima kwa bei elekezi ya soko.

# Samia: Haya hapa maeneo makuu yatakayoibeba nchi kwa kilimo

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA imepanga kuweka nguvu kwenye uwekezaji wa ngano, mafuta ya kula, mazao ya bustani na ufugaji, ikiwa ni sehemu ya maazimio ya Mkutano wa Pili wa Kilimo na Chakula uliofanyika jijini Dakar, Senegal.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wakuu wa nchi 34 za Afrika, mawaziri wenye dhamana ya kilimo na fedha pamoja na magavana wa benki kuu.

Mkutano huo uliandaliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kushirikiana na nchi mwenyeji, Senegal ukiongozwa na Rais wa nchi hiyo, Macky Sall, Tanzania iliwakilishwa na Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la viongozi.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, ilieleza kuwa katika mkutano huo, Rais Samia alieleza umuhimu wa kuwashirikisha vijana katika kilimo kwa kutatua matatizo ya upatikanaji wa ardhi, mitaji, teknolojia na upatikanaji wa masoko.

Rais Samia alisema kundi la vijana ni kubwa, akitoa kwa Tanzania kuwa kundi hilo ni asilimia 34.5 ya idadi ya Watanzania milioni 61.7 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Alisema Dira ya Kilimo ya Tanzania ya ajenda inayolenga kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Alisema kuwa kupitia ajenda hiyo, serikali imeanzisha programu iitwayo BBT ambayo itawapatia vijana maeneo ya ekari 10 kwa kila mtu, yakijumuisha wawekezaji katika mashamba makubwa yenye ukubwa wa kati ya ekari 1,000 hadi 20,000.

Rais Samia alisema wawekezaji hao watawezesha vijana kutumia teknolojia bora na kununua mazao yatakayozalishwa kwenye mashamba ya vijana na kuongeza thamani.

### KILICHOJADILIWA

Wajumbe wa mkutano huo walijadili kwa kina suala la hali ya ongezeko la bei za vyakula duniani kutokana na athari za ugonjwa wa corona, mabadiliko ya tabianchi na vita vya Russia na Ukraine.

Ilielezwa kuwa katika kufikia malengo hayo, unahitajika utashi wa kisiasa na utayari wa serikali na sekta binafsi katika kutekeleza mipango, mikakati na programu za kuendeleza kilimo pamoja na kutoa rasilimali fedha.

### MAAZIMIO YA MKUTANO

Kutokana na majadiliano hayo, mkutano huo ulitoa maazimio mbalimbali, yakijumuisha kila nchi ikamilishe mpango wa uwekezaji katika kilimo kwenye vipaumbele vya taifa uliojadiliwa na wabia wa maendeleo na sekta binafsi wakati wa mkutano huo wa Senegal.

"Kwa Tanzania, vipaumbele vya uwekezaji ni ngano, mafuta ya kula (alzeti), mazao ya bustani (parachichi) na ufugaji (nyama na maziwa)," ilibainishwa katika taarifa hiyo ya Ikulu.

Azimio la pili ni kila nchi kuanzisha kitengo maalum cha Rais kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mpango wa taifa wa kuendeleza kilimo katika vipaumbele vilivyokubaliwa.

Azimio lingine ni kuwezesha utekelezaji wa mpango wa taifa kwa kuainisha muda wa utekelezaji, viashiria vya kupima mafanikio pamoja na kuwa na sera, sheria na vivutio vya uwekezaji katika kilimo.

Lingine ni kuendelea kuratibu upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia mpango.

Azimio lingine ni kuongeza bajeti ya taifa kwa ajili ya kuendeleza kilimo ili kufanikisha mpango ikiwa ni utekelezaji wa azimio la malabo lenye lengo la kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo kwa kutenga angalau asilimia 10 ya bajeti kuhudumia kilimo.

Azimio lingine ni wadau wa maendeleo na taasisi za fedha za kimataifa walionyesha utayari wa kutoa Dola za Marekani bilioni 30 kwa ajili ya kugharamia mipango ya maendeleo ya kilimo kwa nchi za Afrika. Tume ya Umoja wa Afrika na Benki ya Maendeleo ya Afrika walielekezwa kufuatilia upatikanaji wa rasilimali fedha hizo.

# IHC yawekeza Bil. 940/- kwenye kampuni ya Adani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uwekezaji ya International Holding Company (IHC) imetangaza kuwekeza Dola la Marekani milioni 400 (Sh. bilioni 940) kwenye hisa za kampuni ya Adani Enterprises.

Kampuni hiyo kutoka Falme za nchi za Kiarabu imenunua asilimia 16 ya hisa zote za Adani Enterprises kwenye soko la hisa zenye thamani ya Dola milioni 400 zinazogharimu Dola za Marekani bilioni 2.5.

IHC ni kampuni yenye makao makuu Dubai wakati Adani ni kampuni kubwa ya kimataifa ya India.

Taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo ilisema kuwa uwekezaji wa IHC kwenye kampuni ya Adani ni sehemu ya mkakati wake wa kuwekeza kwenye nchi mbalimbali barani Ulaya, Afrika, Asia na Marekani Kusini.

"Uamuzi wetu wa kuwekeza kwenye kampuni ya Adani Group unatokana na imani yetu kwenye misingi ya kampuni ya Adani. Tunaona fursa kubwa ya kukua kwa kampuni hii," Ofisa Mtendaji Mkuu wa IHC, Syed Basar Shueb, alisema katika taarifa yake.

Kampuni ya Adani Group mwezi wa Agosti mwaka jana ilisaini makubaliano ya awali (MoU) na Kampuni ya Abu Dhabi Ports kushirikiana kwenye fursa za uwekezaji nchini Tanzania, ikiwamo maeneo ya Bandari na miundombinu.

Kampuni ya Adani mwaka jana iliwekeza Dola za Kimarekani bilioni mbili katika kampuni tatu kubwa ambazo zimeorodheshwa katika soko la hisa nchini India.

"Faida katika uwekezaji huu ni kutokana na historia ya ripoti ya mapato ya kampuni, uendeshaji, biashara zake na data za kibenki kabla ya kufanya uamuzi wa kuwekeza," alisema Shueb.

Kampuni ya IHC inaendelea na mikakati ya kupata mafanikio katika mabara manne mpaka mwishoni mwa mwaka2023 ikilenga maeneo ya ukuaji haraka wa uchumi, kupanua masoko na maeneo ya uwekezaji.

"Tunaangalia masoko ya kimataifa tukitarajia kuendelea kutafuta fursa zaidi nje ya utamaduni wetu wa soko kwa mwaka 2023," aliongeza Shueb.

IHC imelenga kuongeza mafanikio kwa asilimia 70 katika kipindi cha mwaka huu, kwenye nishati safi na hasa kwenye uchakataji wa mazao.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA Maabara ya Upimaji zege/Simiti**

**KUMBUKUMBU NAMBA: ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE0015**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za Ujenzi wa Gati na Kituo cha Upakiaji katika Ghuba ya Tanga kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

- **Upimaji wa Zege kwenye simiti iliyokwisha tengenezwa punde na simiti ngumu (zege iliyokauka), Upimaji wa awali wa Zege**
- **Upimaji chuma (nondo) kitaalamu**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha. Jeti yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Tangi za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Upimaji wa simiti/zege kulingana na BS EN 206 + A1 ambayo inajumuisha simiti/zege ya awali, iliyotengenezwa upya/punde na ngumu.
- Kukagua zege (mass concrete) kwenye mradi
- Uthibitishaji wa kifuniko cha zege (concrete cover) kwa majenzi ya precast
- Upimaji wa kiwango cha kloridi kutoka kwa simiti/zege iliyochimbwa
- Upimaji wa uimarishaji wa chuma/nondo kulingana na BS EN 10080 na BS 4449

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo.
- Orodha ya uzoefu iliyo na historia ya ugavi / rekodi ya inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma sawa za shughuli za kupima zege na chuma/nondo kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa.
- Vyeti vya ubora/viwango vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na watoa huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi unapendekezwa sana.
- Rasimu/Sampuli ya ripoti katika umbizo la PDF
- Orodha ya vifaa vya kupima saruji/zege
- CV za wafanyakazi/wataalam wa upimaji zege

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma, yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz** (**ukubwa wa barua pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza**) mnamo au kabla ya tarehe **14 Februari 2023, 12:00** jioni Saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA Huduma za Urekebishaji (Calibration) Vifaa vya Ukaguzi na Upimaji**

**KUMBUKUMBU NAMBA: ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE0010**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za ujenzi wa Gati na Kituo cha Upakiaji katika Ghuba ya Tanga kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

- **Huduma ya urekebishaji wa vifaa vya ukaguzi na upimaji (testing & measuring Equipment)**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA UPEO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Urekebishaji wa zana na vifaa vya kufanya ukaguzi wa kuchomelea na mipako
- Urekebishaji wa vifaa vya uchunguzi
- Urekebishaji wa vyombo vya kupimia
- Urekebishaji wa vifaa vya NDT
- Urekebishaji wa viwango vya joto na shinikizo
- Urekebishaji wa zana/vifaa vya kupimia vya HSE (Afya, usalama na Mzingira sehemu ya Kazi)

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo.
- Orodha ya vifaa, chapa (brand) zake na aina ya vyombo ambavyo vitatumika kufanyia huduma ya marekebisho (calibration).
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi / rekodi husika inayoonyesha uzoefu usiopugua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma zinazofanana za urekebishaji unaohitajika kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa.
  Vyeti vya ubora/viwango vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, EN/IEC 17025
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na watoa huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi unapendekezwa sana

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa barua pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **14 Februari 2023, 12:00** jioni kwa Saa za Tanzania,

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

## Serikali yakamilisha mchakato mabadiliko sheria ya habari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema serikali inakamilisha mchakato wa maoni ya wadau kwenye Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari 2016 na rasimu itakabidhiwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, pamoja na mambo mengine Nape alisema ni muhimu wadau wakashiriki kutoa maoni yao kwa kuwa wapo kwenye hatua za mwisho za mabadiliko ya sheria hiyo.

"Wizara imekamilisha utaratibu na kuwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa ajili ya kuendelea na mchakato wa kuwasilisha bungeni,"alisema Nape.

Wakati huo huo, alisema wizara imeunda timu ya kutathmini hali ya uchumi wa vyombo vya habari na waandishi wa habari nchini, ili kukwamua tasnia ya habari itakayofanyakazi kwa miezi mitatu.

Alisema Mwenyekiti wa timu hiyo ni Tido Mhando ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Azam Media group na itafanya kazi kwa muda usiozidi miezi mitatu.

"Rais alipoingia madarakani alionyesha kutoridhishwa kwake na hali ya waandishi wa habari hasa kwenye uchumi wa waandishi wa habari na vyombo vya habari, aliponiapisha aliniagiza moja ya mambo ya kushughulikia ni hili."

"Tumekuwa na majadiliano ndani ya wizara na nje ya wizara, tumefikia mahali tumesema sasa tuunde timu itakayotokana na wanahabari wenyewe itakayokwenda kufanya kazi ya kutathmini hali ya uchumi kwa vyombo vya habari na wanahabari wenyewe halafu italeta mapendekezo," alisema.

Kadhalika, alisema baada ya kutafakari na kupata taarifa mbalimbali serikali imefikia uamuzi wa kuunda timu hiyo ambayo itafanya majukumu mbalimbali, ikiwamo kupata taarifa ya hali ya vyombo vya habari kiuchumi na kiutendaji.

"Sasa kamati hii ifanye kazi ya kupata hali ya vyombo vya habari kiuchumi na kiutendaji, pia watafanya kazi ya kupata taarifa ya hali ya waandishi wa habari katika vyombo vya habari ikiwamo walioajiriwa, wenye mikataba, wawakilishi mikoani na wanaoshirikiana nao kwenye kazi za habari," alisema. Alisema katika suala la mikataba timu hiyo itapaswa kupeleka taarifa namna mikataba inavyoheshimiwa, watatathmini sababu ya tatizo la kiuchumi kwenye vyombo hivyo.

"Watapendekeza njia bora ya kukabiliana na changamoto hizo, yapo ambayo yatatekelezwa na vyombo vyenyewe vya habari, yapo ambayo yatatekelezwa na serikali na kama kuna mdau yeyote ambaye anataka kutekeleza jambo ili uchumi wa vyombo vya habari uende sawa sawa tutapokea hayo mapendekezo," alisema.

Aliwataja wajumbe wengine Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Gerson Msigwa, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, Mkurugenzi Mtendaji wa ITV na Radio one, Joyce Mhavile, Mkuu wa Maudhui Clouds Media Group, Sebastian Maganga, Mtendaji Mkuu wa Mwananchi Communication, Bakari Machumu.

Wengine ni Mkurugenzi wa Umoja wa Vilabu vya Waandishi wa Habari (UTPC), Kenneth Simbaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Multichoice Tanzania, Jackline Woiso na Mwandishi wa habari mkongwe, Richard Mwaikenda.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
30.01.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 03-02-2023** kampuni ya **Spedag Interfreight Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga** kupitia **Mlandizi** gari hizo zina namba za usajili:
   **NRB 69149 / NRB 15200**
   **DS00TG-GP / NRB 53910**

2. Garihizozinavipimovifuatavyo:
   **Urefu - mita 28.00**
   **Upana - mita 5.40**
   **Kimo - mita 4.70**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Mzenga kupitia Mlandizi** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

117256302

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


## JKCI: Wengi wanafika hospitalini moyo wao uko dakika za mwisho

**Na Christina Mwakangale**

IMEBAINISHWA kuwa Watanzania wanaofika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kupata matibabu ya moyo, kiwango cha ufanyaji kazi wa kiungo hicho muhimu kinakuwa kimechoka huku baadhi yao kufikia asilimia 25 hadi 17.

Kaimu Mkurugenzi wa JKCI, Dk. Anjela Muhozya, amesema taasisi hiyo imekumbana na changamoto hiyo mara kadhaa kutoka miongoni mwa wagonjwa inaowatibu na kwenye kambi za upasuaji zinazowekwa kwenye maeneo tofauti nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam baada ya kufanyika upasuaji wa kifua kwa tundu dogo, Dk. Anjela alisema upasuaji huo umefanywa na madaktari bingwa wa JKCI kwa kushirikiana na wenzao kutoka Hospitali ya Max ya India.

"Watanzania wengi wanakuja kupata matibabu ya moyo wakati kiwango cha moyo wao kufanya kazi kimechoka sana na katika kambi hii tumekutana na mgonjwa ana kiwango cha asilimia 17.

"Kwa wenzetu India na nchi zilizoendelea, matibabu hufanyika bila shida kwa sababu ya uzoefu na vifaa. Pia madaktari wetu wamejifunza nini kifanyike kwa wagonjwa wa aina hii," alisema Dk. Anjela.

Alisema ushirikiano na mabingwa kutoka nje, hugusa eneo ambalo wataalamu wa ndani hawajalifikia ama kufanya upasuaji wa aina fulani na kwamba sasa ni mwaka wa pili hospitali hiyo inashirikiana na JKCI.

Bingwa wa Moyo kutoka Hospitali ya Max, Dk. Subhash Sinha, alisema kwamba kutokana na ushirikiano huo, anaona timu inaendelea kukuza ujuzi, akisema jambo muhimu ni kujifunza kutokana na makosa.

Bingwa wa Upasuaji wa Moyo na Mishipa wa JKCI, Dk. Evarist Nyawawa, alisema upasuaji uliofanyika ni wa kupandikiza mishipa na mabingwa kutoka nje wanapoalikwa uzoefu huongezeka.

"Kwa kipindi kifupi alipofika mtaalamu huyo, wagonjwa wanane wamefanyiwa upasuaji wa kupandikiza mishipa na kama wangepelekwa India ingegharimu Sh. milioni 360.

"Na hata atakapoondoka timu ya wazawa itaendelea na upasuaji huu kwa sababu timu imeshapata uzoefu kwa kiwango kikubwa," alisema Dk. Evarist.



Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Hawa Msuya (wa pili kushoto), Meneja wa Benki ya CRDB Tanga, January Kirambata, pamoja Ofisa Elimu ya Awali na Msingi, Kassim Kaoneka (walioketi katikati), wakiungana na wanafunzi wenye uhitaji maalumu kuipongeza Benki ya CRDB kwa msaada wa madarasa mawili katika Shule ya Msingi Chuda jijini humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mloganzila yabaini ongezeko mara tano wagonjwa wa akili

**Na Maulid Mmbaga**

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Afya ya Akili Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila, Dk. Fileuka Ngakongwa, amesema idadi ya wagonjwa wa akili wanaopokewa, inazidi kuongezeka kutoka wastani wa watano hadi 25 kwa siku.

Akizungumza na Nipashe hospitalini huko mwishoni mwa wiki iliyopita, Dk. Fileuka alitaja visababishi vya ugonjwa wa akili kuwa ni ulevi wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya kama bangi na heroin.

Alibainisha kuwa miongoni mwa wanaopokewa hospitalini huko wanabainika baada ya uchunguzi wa kitabibu, kwa asilimia kubwa walitumia vilevi hivyo na kuwa kiini cha matatizo yao.

Kichocheo kingine kwa mujibu wa bingwa huyo, ni msongo wa mawazo, tatizo la hisia na wasiwasi uliopitiliza.

Alisisitiza umuhimu wa kutoa elimu kwa jamii na shuleni kwa kuanza na wanafunzi wa chini ambao hawajafikia umri mkubwa ili wasipate mhemko wa kuanza kutumia dawa hizo.

"Elimu katika jamii na shuleni ni muhimu sana, tuone kwamba mtoto wa mwenzako ni wako, tuwahudumie bila kuwanyanyapaa, hii itasaidia kupunguza tatizo la matumizi ya mihadarati," alishauri Dk. Fileuka.

Pia aliitaka jamii kutowanyanyapaa wenye tatizo la akili na badala yake iwahudumie na kutoa ushirikiano kwa wataalamu wanaowapatia matibabu kwa kuwa tiba ipo na mtu anaweza kutibiwa na akapona.

Kuhusu vikwazo wanavyopitia, bingwa huyo aliutaja uhusiano wa familia na madaktari katika kumtibu mgonjwa, akisisitiza jamii na familia zenye watu wenye tatizo hilo, kujitoa na kuwa na uwezo wa kumsaidia mgonjwa wao kwa pamoja.

"Familia na jamii kwa pamoja iwe na uwezo wa kusaidia kwa pamoja ili kumsaidia mgonjwa wetu na tusimnyanyapae katika jamii, kwa sababu ukifanya hivyo 'ndo' kunakuwa na ile hali ya kila mtu kujificha, hataki kwenda hospitalini.

"Tukiweza kuondoa ile hali ya kumnyanyapaa katika jamii au familia, inakuwa ni rahisi zaidi kuwatibu na kupunguza magonjwa haya," alisema Dk. Fileuka.

Alisema hospitali hiyo inatoa huduma za kila nyanja ikiwamo tiba ya dawa, mazungumzo, tiba kazi na za kijamii na kwamba katika utoaji wa huduma za matibabu, wanashirikiana na wasaikolojia tiba.

Mbali na huduma hizo, bingwa huyo alisema pia wanatoa huduma zingine kwa wenye changamoto kupita kiasi na kwamba kwa wale ambao tiba ya dawa haijafanya kazi, wanapatiwa huduma aliyoitaja kwa jina la ECT, akifafanua kuwa inajumuisha matumizi ya umeme mdogo kwenye kichwa ili kuchangamsha ubongo.

"Hapa tunapokea wagonjwa ambao wako katika hali ya hatari ambao tunawafanyia tiba za mwendelezo," alibainisha Dk. Fileuka.

TANGAZO

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

MuCoBa Bank PLC
"Kwa Maendeleo Yako"

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31-12-2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 31/12/2022 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 30/09/2022 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 240 | 895 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 13 | 115 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 2,393 | 2,522 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 15,699 | 15,294 |
| 12 | Mali nyingine | 3,829 | 4,492 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 555 | 565 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **22,730** | **23,884** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 14,060 | 14,716 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 87 | 117 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 178 | 152 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 233 | 525 |
| 28 | Madeni | 3,776 | 3,526 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **18,337** | **19,040** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **4,393** | **4,844** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 8,789 | 8,789 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (5,098) | (4,536) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 535 | 425 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | 166 | 166 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| **37** | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **4,393** | **4,844** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,509 | 1,470 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 140 | 140 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 19.33% | 20.03% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 9.87% | 9.61% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 116.09% | 107.99% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 69.07% | 64.04% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 89.51% | 87.20% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -4.63% | -1.49% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -4.83% | 2.20% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-12-2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 31/12/2022 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/09/2022 | Limbikizo lamwaka sasa 30/12/2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30/09/2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 744 | 829 | 3,102 | 3,871 |
| 2 | Gharama za Riba | (226) | (185) | (734) | (665) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 518 | **644** | 2,368 | 3,206 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | 20 | (190) | (374) |
| | | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 262 | 250 | 968 | 831 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 262 | **250** | 968 | 748 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | 82 |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | (671) | **(672)** | (2,612) | (2,763) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (374) | (371) | (1,457) | (1,344) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | (35) | - | (213) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (297) | (266) | (1,155) | (1,207) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | 109 | 222 | 534 | 899 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (30) | (30) | (120) | (120) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | 79 | 192 | 414 | 779 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | 79 | **192** | 414 | 779 |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 55 | 55 | 55 | 60 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 2.42 | 5.88 | 13 | 26 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 0.47% | 0.95% | 2.29% | 3.80% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 2.38% | 4.84% | 2.91% | 3.80% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 66.70% | 62.27% | 64.18% | 20.40% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 2.79% | 3.47% | 5.67% | 58.78% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho
kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31-12-2022
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Mwaka wa sasa 2022** | | | | |
| | **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,795** | **(4,558)** | **107** | **4,345** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 534 | - | 534 |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | 21 | - | 21 |
| | Miamala na Wanahisa | (6) | - | - | (6) |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| | Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | (501) | - | (501) |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(4,503)** | **107** | **4,393** |
| | | | | | |
| | **Mwaka Uliopita 2021** | 8,886 | (5,280) | 87 | 3,693 |
| | Salio la mwanzo wa mwaka | - | 743 | - | 743 |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | (91) | - | - | (91) |
| | Miamala na wanahisa | - | - | - | - |
| | Gawio lililolipwa | - | (20) | 20 | - |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| | Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,795** | **(4,558)** | **107** | **4,345** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-12-2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 31/12/2022 | Robo ya Mwaka iliyopita 30/09/2022 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31/12/2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31/12/2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 109 | 222 | 534 | 899 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | - |
| | Hasara Katika Mali | 91 | 70 | 509 | 574 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (407) | 432 | (839) | (1,462) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (687) | (224) | (2,261) | 1,211 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (266) | (68) | (597) | (115) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 662 | (91) | 629 | (972) |
| | Kodi Iliyolipwa | (30) | (30) | (120) | (239) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **(528)** | **311** | **(2,145)** | **(104)** |
| | | | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (48) | (32) | (122) | (117) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(48)** | **(32)** | **(122)** | **(117)** |
| | | | | | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 250 | (100) | 1,249 | (260) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (562) | 177 | (471) | (91) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **(312)** | **77** | **779** | **(351)** |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | (887) | 356 | (1,488) | (572) |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 3,533 | 3,177 | 4,141 | 4,713 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **2,646** | **3,533** | **2,653** | **4,141** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Philip Raymond .................................. Meneja Mkuu | (Imesainiwa) | 30/Jan/2023 |
| Kelvin Mushi ..................................... Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | (Imesainiwa) | 30/Jan/2023 |
| Saleh S. Abdallah................................. Mkaguzi Mkuu wa Ndani | (Imesainiwa) | 30/Jan/2023 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | Tarehe |
|---|---|
| 1. Arafat A. Ally...................... (Imesainiwa) Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | 30/Jan/2023 |
| 2.. Bakar R. Bakar ....................... (Imesainiwa) Mkurugenzi | 30/Jan/2023 |

## DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2015

## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

**MUCOBA BANK PLC- REVISED CHARGES AND FEES- SEPTEMBER 2021**

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 2,000 |
| Credit Interest Rate | 1% pa |
| | |
| **Group Savings Account (GS09)** | |
| Account opening minimum amount | Free |
| Minimum operating balance | Free |
| Minimum Interest-Bearing balance | N/A |
| Cash Withdrawal Fee | Refer cash withdrawal fee below |
| Credit Interest Rate | N/A |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 2,000 |
| Credit Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 10,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 2,000 |
| Interest Rate | |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |
| Prematurity withdrawals | 10,000 |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | Rate |
|---|---|
| 3 months | 4% |
| 6 months | 5% |
| 12months | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs**10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 3,000 |
| Cash withdrawal- from Tzs 5,000,000 and above) | 3,000+0.12%, Max Tzs 150,000 |
| Account closure | 10,000 |
| Dormant account reactivation | 5,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,500 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Bank Statement Fee /page | 2,000 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | 15,000 |
| TT Outward local- EFT | 15,000 + Levy |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Inward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balance Inquiry:<br>*Mobile banking<br>*Over the counter<br>*ATM | <br>200<br>500<br>400 |
| Money Transfer | 15,000 |
| ATM card | 15,000 |
| Searching Fee | 10,000 |
| Coins deposit fee | 10% |
| ATM card replacement | 10,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,500 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,500 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alert | 500 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |
| ATM Balance Inquiry | 400 |
| Annual card maintenance fee | 5,000 |
| PIN re-issue | 1,000 |
| Card replacement fee | 15,000 |
| Monthly fee | 2,000 |
| Standing Order | 10,000 |

**LOAN CHARGES AND COMMISION**

| S/NO | LOAN PRODUCTS | CHARGIES |
|---|---|---|
| 1. | 1.Business loan<br>2.Mixed loan<br>3.Agriculture loan<br>4.Housing loan<br>5.Assets acquisition loan | -Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 20,000/=<br>-Delay fines 0.1<br>-Interest rate<br>A. 1-6 Months 13% pa<br>B. 7-12 Months 18% pa<br>C. Above 12Months 20% pa |
| 2. | 1.Group loans | -Application fee 1%<br>-Interest rate 25% pa |
| 3. | 1.Salary loan full guarantee- Government | - Indemnity fund 3% of the approved amount.<br>-Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 10,000/=<br>-Interest rate 13% pa |
| 4. | 1.Salary loan full guarantee- Private sector | - Indemnity fund 3% of the approved amount.<br>-Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 10,000/=<br>-Interest rate 14% pa |
| 5. | 1.MUCOBA staff loan | - Indemnity fund 3% of the approved amount.<br>-Interest rate 5% pa |

2172567O2

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanawake waongoza kufungua mashauri ya mirathi

**KITUO** Jumuishi cha Utoaji Haki Temeke, kilitoa takwimu kuonesha kwamba wanawake wanaongoza kwa kufungua mashauri ya ndoa, talaka na mirathi.

Kituo hicho kimeshahudumia mashauri 100,484 tangu kianzishwe, Oktoba mwaka jana.

Imeelezwa kuwa mashauri 55,773 ambayo ni sawa na asilimia 54 yalifunguliwa na wanawake, hali inayoonesha kuwa wengi wao wanajua umuhimu wa kudai haki zao kupitia njia sahihi za utoaji haki hasa linapotokea suala la ndugu kugombea mirathi.

Jaji Mfawidhi wa Mahakamu Kuu Kanda ya Temeke, Ilvin Mgeta, anafafanua kuwa idadi hiyo kubwa ya wanawake inatokana na wengi wao kupitia wakati mgumu wanapofiwa na waume zao kwenye masuala ya mali tofauti na wanaume wanapofiwa na wake zao.

Hali ya kugombea mali mwanamke anapofiwa na mume, hasa kutoka kwa ndugu wa mume ndiyo sababu mashauri ya wanawake kuwa mengi, kwa mujibu wa Jaji Mgeta.

"Kwa kuona hali hiyo ndiyo maana tunaweka mazingira mazuri kumsaidia huyu mwanamke aliyeumizwa na huu mchakato anaopitia baada ya kufariki kwa mume wake asikilizwe bila upendeleo, lakini aridhike kwamba ametendewa haki."

Kwa mujibu wa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Temeke, Mary Moyo, mpaka wiki hii Ofisi ya Ustawi wa Jamii wa kituo hicho, imehudumia watu 1,329 wakiwamo wanawake 901 sawa na asilimia 68 na wanaume ni 428 ambayo ni sawa na asilimia 42.

Hata hivyo, hoja kwamba wanawake wanaonekana kupendelewa kwenye kituo hicho, ilielezwa kuwa haina ukweli kwa kuwa wengine wao ndiyo wanaofika kufungua mashauri kutokana na kupata matatizo wanapotelekezwa na watoto.

Huduma zinazotolewa na wadau mbalimbali wa Ustawi wa Jamii zinaonyesha kwamba idadi ya wanawake ni kubwa kulinganisha na wanaume kutokana na mazingira wanayopitia.

Inasemekana kuwa wanaume wengi hawajitokezi kudai haki zao kwa kuogopa fedheha au kuchekwa, hali inayosababisha waendelee kuumia na wengine kupoteza maisha kwa sababu ya msongo wa mawazo.

Kituo hicho kimeshatoa huduma kwa watu 2,811 na kati yao wanawake ni 1,878 sawa na asilimia 66 na 933 ni wanaume ambao ni sawa na asilimia 34.


"Sisi hatumpendelei mwanamke kwenye utoaji wa haki isipokuwa tunaweka mazingira wezeshi ili hata lile kundi linaloonekana kuwa nyuma liwe katika mazingira sawa kwenye mchakato wa kupata haki na kwenye masuala haya mwanamke ndiye mwathirika zaidi ya mwanaume."

Katika hili, hakuna budi wananchi hasa wanaume kuhudhuria mahakamani kila wanapoitwa ili iwe rahisi kutenda haki kutokana na uzoefu kuonesha baadhi ya watu wamekuwa wakipuuzia wito wa mahakama na mwisho haki inapotolewa upande uliokuwa ukihudhuria kunakuwapo malalamiko kwamba haki haikutendeka na upendeleo.

Wahenga walisema usikatae wito kataa neno. Wananchi wanapoitwa kwenye mashauri ni lazima wawe wanatii wito kwa kufika mahakamani kwa wakati ili haki itolewe kwa wakati mfupi na wahusika waendelee kwenye shughuli zao za uzalishaji mali badala ya kila siku kushinda mahakamani kusikiliza mashauri.

Kunapokuwapo na pande zote mbili kwenye mashauri ni rahisi kupata suluhisho na haki kutolewa bila kuwapo malalamiko kuwa kuna upendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Elizabeth Zaya

# 'Wanasheria wasomi anzeni kujitafakari'

**SEKTA** ya sheria ndiyo inayosimamia kwa kiwango kikubwa haki za watu katika maeneo mengi kuanzia uchumi, siasa, elimu hadi mirathi.

Tanzania inaadhimisha wiki ya sheria ambayo Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, ameizindua hivi karibuni na kueleza namna ambavyo amekuwa akipokea malalamiko mengi ya wananchi dhidi ya vyombo vinavyohusika na utoaji wa haki ikiwamo mahakama, polisi na magereza.

Na miongoni mwa malalamiko anayoyataja ni baadhi ya mahakimu, mawakili na majaji wasiowaaminifu wanavyodai rushwa, wengine wakiwatoza watu gharama kubwa za kuendesha kesi hasa mawakili.

Kingine alisema kumekuwapo na wananchi kulalamikia suala la kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza, lakini watuhumiwa kukaa kwa muda mrefu wakisubiri uchunguzi kukamilika.

Nasema kwamba hayo yaliyotajwa na Dk. Mpango ni nyeti na japokuwa bado yapo mengine ambayo huenda yanapuuzwa licha ya kuwa yamebeba hatima ya maisha ya watu, wahusika ni lazima watafakari njia zao.

Wapo wanaokubaliana na mimi kuwa vitabu vitakatifu vimeonya wanasheria kuwa hawatamwona Mungu ni kutokana na upotoshaji, upindishaji na rushwa ili kuwanyima haki wanaostahili hasa wanyonge.

Pamoja na hayo yaliyotajwa na kiongozi mkuu wa nchi wakati akifungua wiki hii muhimu ya sheria, kipekee naomba kuongezea katika eneo la mashauri ambayo yamekuwa yakiwasilishwa katika vyombo hivyo kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Hili nalo ni miongoni mwa maeneo ambayo yanahitajika kuja na mkakati madhubuti hasa wa kisheria wa kulitatua tatizo hilo, kama si kulikomesha.

Kwa sasa kila kona ni vilio vya watoto kufanyiwa ukatili ambavyo vimetanda, watoto wengi wanabakwa, kulawitiwa huku wakiumizwa kimwili na kisaikolojia.

Kesi za watu wanaofanya vitendo hivyo ni 'kizungumkuti' ni eneo linalonuka rushwa, hata zile kesi zinazoripotiwa katika vyombo vya maamuzi hazifiki mbali, baadhi ya watuhumiwa wamekuwa wakitumia nguvu ya fedha kuzimaliza.

Hata mashahidi wanapojitokeza, wengi wao wamekuwa wakitishwa wasiseme au kutoa ushahidi kutoka kwa wenye nguvu ya fedha.

Kama hiyo haitoshi, pia, kutokana na kuwa na mlolongo mrefu wa kupatikana kwa haki katika vyombo vinavyohusika na utoaji wa haki hiyo, baadhi ya wazazi au walezi hufikia hatua wanakata tamaa ya kufuatilia kesi zinazohusu watoto wao kufanywa vitendo vya ukatili.

Ikumbukwe kwamba ukatili dhidi ya watoto una athari kwa maendeleo ya mtoto kihisia, kitabia, kimwili na unaharibu maendeleo yake ya kijamii na maisha yake yote.

Watoto wengi wanafanyiwa vitendo vya kikatili na unyanyaswaji na hivyo kusababisha kushindwa kufurahia utoto wao na kuwaletea madhara makubwa kiakili, kihisia na kimwili.

Hali hii isipokomeshwa itaendeleza mzunguko wa umaskini na ukatili katika jamii zetu. Au taifa litakosa viongozi au kuwapata watu ambao watakuwa siyo wazalishaji mahiri na hata kukaribisha mmomonyoko wa maadili.

Sheria ya mtoto inamtaka mtu yeyote mwenye sababu ya kuamini kuwa mtoto amefanyiwa ukatili na unyonyaji, kutoa taarifa juu ya jambo hilo. Jamii yote ina jukumu la uhakikisha kwamba watoto wanalindwa.

Ni kilio cha wazazi na wanajamii kuona hili nalo linatupiwa jicho la tatu na kupatikana suluhisho lake kwa kudhibiti. Sheria ya Mtoto ya 2009 inaeleza kwamba mtoto anahitaji malezi bora ili aweze kuishi vizuri, kushirikishwa , kulindwa na kuendelezwa kiakili kwa ajili ya maisha yake ya baadaye ya utu uzima.

Hivyo basi, katika wiki hii ya sheria niombe wadau katika sekta hii nyeti ya kutoa haki, ilijadili jambo hili na kisha majibu ambayo yataleta mwanga kukomesha ukatili kwa kundi hili la watoto yapatikane. Na ikibidi hata bunge nalo kwa sehemu yake kwa vikao vinavyotarajia kuanza hivi karibuni itoe neno la matumaini katika janga hili.

# Waziri na mbunge wakoshwa na mikakati mgodi kusaidia jamii

**Na Faustine Feliciane,** KAHAMA

MBUNGE wa Msalala mkoani Shinyanga, Iddi Kassim Iddi, amesema uhusiano mzuri uliopo kati ya wananchi na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu mkoani Shinyanga, umeusukuma mgodi kutoa zaidi ya Sh. bilioni tisa kwa ajili ya maboresho ya barabara kutoka Kakora hadi Kahama.

Akizungumza kwenye mkutano wa uongozi wa juu wa mgodi, Wizara ya Madini, viongozi wa Mkoa wa Shinyanga na viongozi wa vijiji vinavyozunguka mgodi huo, Mbunge Iddi alisema mgodi huo umetekeleza ahadi ya kusaidia vijiji vinavyozunguka mgodi huo kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, vituo vya afya na shule.

Alisema mbali na kujenga miundombinu na kuweka vifaa kwenye Kituo cha Afya Bugarama, mgodi huo pia umetoa dola milioni 40 (zaidi ya Sh. bilioni 90) kwa ajili ya ujenzi wa barabara inayounganisha maeneo hayo na Manispaa ya Kahama kutoka Kijiji cha Kakora hadi mjini Kahama.

Alisema barabara hiyo itarahisisha huduma za kijamii kati ya Msalala na Kahama, pia kuchochea fursa za kibiashara kwa wakazi wa maeneo hayo.

"Hii ni faida ya kuwapo mgodi huu, wakazi wa maeneo haya tunaona kile kinachofanywa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu.

"Hii yote ni juhudi za serikali kuhakikisha kuwapo kwa mgodi huu kunanufaisha taifa na hasa wakazi wa maeneo yanayozunguka mgodi huu," alisifu Iddi.

Alisema kuwa kwenye Kituo cha Afya Bugarama, Barrick imejenga jengo la wazazi na jengo la kuhifadhi maiti na kuweka vifaa vya X-ray na Ulta sound.

"Huko nyuma wananchi wa maeneo haya ya Bugarama na Msalala kwa ujumla walikuwa wanalazimika kwenda Hospitali ya Wilaya ya Kahama kufuata huduma za X-ray na Ulta-Sound, lakini kwa sasa hatuhitaji tena kwenda Kahama kutafuta huduma hizi kwa sababu ya vifaa vyote muhimu kwenye kituo chetu cha afya ya Bugarama vipo," alisema Iddi.

Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Silas Kayanda, alisema kuimarishwa kwa hospitali hiyo kumesaidia kupunguza vifo vitokanavyo na ujauzito kutoka vifo zaidi ya vitatu kwa mwaka, sasa wakirekodi kimoja kwa mwaka jana.

"Kuna vijiji 14 kutoka kata tatu za Bugarama, Bulyanhulu na Kakora ambavyo vinaitegemea hospitali hii, huko nyuma wananchi walilazimika kwenda Kahama kufuata huduma ambazo hapa tulikuwa hatuna, lakini kwa sasa kuwapo kwa mashine ya kisasa ya X-ray, Ulta sound na majengo mapya yaliyojenga, kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuwapunguzia mzigo wananchi wa kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hii, kipekee tunaishukuru Barrick na serikali," alipongeza Dk. Kayanda.

Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa, alisema serikali inaridhishwa na juhudi za Mgodi wa Barrick kuboresha miundombinu kwenye sekta za afya, elimu na barabara kwa maeneo hayo ya mgodi.

"Hizi ni juhudi za serikali kuhakikisha kuwapo kwa migodi hii kunanufaisha Watanzania, tunawapongeza sana Barrick kwa juhudi hizi," alisema.

Mtendaji Mkuu na Rais wa Barrick Gold Mine, Mark Bristow, alisema watafanyia kazi changamoto ya kukosekana kwa gari la kubeba wagonjwa kwenye kituo hicho cha afya.

"Kuhusu kuzungusha ukuta kwenye kituo hiki, ninadhani tungeanza na fedha za Mfuko wa Kusaidia Jamii (CSR) zinazotolewa na mgodi kwa wilaya hii, lakini ulinzi unaanzia kwetu wenyewe, tusihujumu miundombinu ya kituo hiki," alisema Bristow.



Balozi wa Fistula wa CCBRT kutoka Mkoa wa Rukwa, Frank Chambika, akipokea cheti kwa Mkurugenzi wa Idara ya Rasilimaliwatu wa Hospitali ya CCBRT, Anastasia Melis, cha kutafuta na kuwafikisha wagonjwa wa fistula hospitalini hapo kwa ajili ya matibabu Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali Wilaya yaanza kutoa huduma ya upasuaji

**Na Kulwa Mzee**

HOSPITALI ya Wilaya ya Ilala (Kivule) imeanza kutoa huduma ya upasuaji na ya mama na mtoto baada ya serikali kufunga vifaa vyote vinavyohitajika.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kivule, Amos Hangaya, alibainisha hayo jana alipozungumza na wananchi wa kata hiyo kuhusu maendeleo yaliyofanyika ndani ya kata yao.

"Tunaipongeza serikali kwa kazi inazofanya. Kwa sasa wakazi wa Kivule na maeneo mengine hawatapata shida ya kwenda mbali kutafuta huduma za afya, huduma zote za matibabu zinapatikana kwenye Hospitali ya Wilaya.

"Vifaa vyote vya upasuaji vimeshafungwa, upasuaji umeanza wiki hii, huduma ya mama na mtoto inapatikana," alisema Hangaya.

Alisema tayari kuna wodi ya wanaume wanaohitaji huduma za kulazwa na sasa wanaendelea na ujenzi wa jengo la kuhifadhi maiti, jengo la kuchomea taka na majengo mengine.


"Zililetwa zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo, tunashukuru kazi inaendelea vizuri chini ya usimamizi wa bodi na Mganga Mfawidhi wa hospitali," alisema. Katika hatua nyingine, kiongozi huyo alihamasisha wananchi kutunza mazingira na kutoa ushirikiano kwa wazoa taka wanapofika kukusanya taka.

Aliomba wenye nyumba zenye mageti, watoe ushirikiano kwa kutoa taka ndani ya nyumba zao na kulipia huduma hiyo kwa wakati kila inapofika mwisho wa mwezi.

"Tulikuwa na mkandarasi wa kuzoa taka, lakini mkataba wao umeisha, tumeweka kampuni nyingine, tunaomba muwape ushirikiano," alisema Hangaya.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# RITA yaelimisha umuhimu kuasili mtoto kisheria

**Na Asha Bani,** DODOMA

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umeelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuasili mtoto kisheria ili kumwezesha kupata mahitaji ya msingi katika jamii.

Ofisa Sheria kutoka RITA, Emmanuella Mwingira, akizungumza katika wiki ya sheria iliyofanyika jijini hapo, alisema, watu wengi hawafahamu umuhimu wa kufuata hatua za kisheria ili kuasili mtoto, katika maadhimisho hayo wanatoa elimu hiyo kwa kina ili kuondoa sintofahamu hiyo katika jamii.

"Inafahamika kuwa katika jamii yetu ya kitanzania wapo watoto wanaokulia katika vituo vya kulelea watoto yatima ama kwasababu ya wazazi kufariki, hawajulikani walipo au hawana uwezo wa kuwapatia matunzo vivyo hivyo wapo watu wazima ambao wanashauku ya kuwa na mtoto hata wa kuasili na hiyo ni kwasababu ya pengine kutojaaliwa kuwa na watoto wa kuwazaa, lakini pamoja na hayo ni muhimu kufuata sheria ili kuasili mtoto rasmi," alisema Emmanuella.

Alisema jumla ya vyeti 975 vimesajiliwa na RITA kutokana na watu mbalimbali kuleta maombi yao ya kutaka kusajili cheti cha kuasili mtoto na kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 imeweka utaratibu wa kusaidia watu wenye uhitaji.

"Kuasili mtoto kisheria ili kupata matunzo ya kudumu ya kifamilia ambapo suala hilo linasimamiwa na sheria ya kuasili Sura ya 335 toleo la mwaka 2002."

"Hata hivyo ili kusajili cheti cha kuasili mtoto kisheria katika ofisi za RITA mwombaji anapaswa kuwasilisha nakala ya uamuzi kutoka Mahakama Kuu na pia cheti cha kuzaliwa cha mtoto anayeasiliwa ili kumwezesha kupata mahitaji yake ya msingi kama elimu, chakula, malazi na masuala ya afya kwa ujumla kama watoto wengine wanavyopata katika jamii." Alisema moja ya haki za mtoto ni kulindwa jambo ambalo watoto wasiokuwa na wazazi wamekuwa wakiteseka kwa kuishi mazingira ambayo sio rafiki, hayana ulinzi na kusababisha kufanyiwa vitendo viovu na watu wasiokuwa na maadili kama kubakwa, kunyanyaswa kijinsia.

Alisema iwapo mtu atasajili cheti cha kuasili sheria itamchukulia kuwa ni sawa na mzazi halisi wa mtoto husika hivyo itasaidia pia kupunguza wimbi la watoto wa mitaani linalokuwa kila kukicha.

"Hii itasaidia pia kwa serikali kupata takwimu sahihi ya wananchi wake katika kupanga mipango mbalimbali ya kimaendeleo katika jamii kama elimu."

RITA pia inatoa huduma ya msaada wa kisheria kuhusu usimamizi wa mirathi, kuandika na kuhifadhi wosia, elimu ya ufilisi, ndoa, talaka, usajili wa cheti cha kuzaliwa pamoja na maelezo ya kina kwa bodi za wadhamini wa taasisi kuhusu namna ya kuhuisha katiba zao.



Kaimu Mhandisi Mkazi wa mradi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere, Justus Mtolera, akifafanua jambo kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme nchini, (TANESCO) alipotembelea mradi huo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wapewa mwongozo kulinda mazingira

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imewaagiza wamiliki wa maeneo ya uchenjuaji dhahabu wanaotumia zebaki na sodium cyanide kujenga mifumo iliyosanifiwa ikiwamo mitaro na sehemu ya kuhifadhi mabaki ili kusiwe na kemikali inayoenda kwenye vyanzo vya maji na kusababisha madhara kwa binadamu na viumbe.

Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula, alitoa agizo hilo jana wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya wachimbaji wadogo wa madini wa mikoa ya Dodoma na Singida yaliyohusu usalama, afya, uhifadhi na usimamizi wa mazingira na matumizi ya baruti.

Prof. Kikula alisema shughuli za uchenjuaji wa dhahabu kwa kutumia zebaki zimekuwa zikisababisha madhara kwa binadamu na viumbe maji yenye mchanganyiko na zebaki yanapotiririka kwenye vyanzo.

Aidha, aliwaagiza maofisa madini wote nchini na wamiliki wenye leseni kuhakikisha hakuna mashimo yanayoachwa wazi ili kuwa na usalama na katika eneo hilo.

Aliwataka wachimbaji madini kutambua kuwa sekta ya madini inaendelea kukua na kuchangia asilimia 10 katika Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025, hivyo wana wajibu wa kuendelea kufanya shughuli za uchimbaji kwa kufuata sheria na kanuni zake.

"Ikumbukwe kuwa zaidi ya asilimia 90 ya mapato yote ya Wizara ya Madini yanatokana na makusanyo ya mrabaha na ada ya ukaguzi, hivyo migodi inaposimama kufanya kazi kutokana na ajali inahatarisha mapato ya wizara na serikali kwa ujumla," alisema.

Aliongeza kuwa wachimbaji wa madini ni wadau muhimu wa maendeleo katika sekta ya madini, wanawajibika kuchangia shughuli za maendeleo katika vijiji wanavyofanyia kazi kwa mujibu wa sheria.

Lengo la mafunzo hayo ilikuwa kuwakumbusha wajibu wao katika kuhakikisha shughuli za uchimbaji na biashara za madini zinafuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa kwa ajili ya uchimbaji endelevu na wenye tija.

# China kupanua kasi kuimarika tena kwa uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

BEIJING, China itafanya juhudi za kupanua kasi ya kuimarika tena kwa uchumi, kuharakisha kufufuka kwa matumizi ya ununuzi na kuleta utulivu wa biashara ya nje na uwekezaji, kwa mujibu wa maamuzi yaliyotolewa kwenye mkutano wa utendaji wa Baraza la Serikali la China ulioongozwa na Waziri Mkuu Li Keqiang, Januari 28, mwaka huu.

Kwa mujibu wa tovuti ya gazeti la umma, kwa kuzingatia mwenendo unaoendelea wa kufufuka kwa uchumi na kuimarika tena, mkutano huo umesisitiza haja ya kutekeleza maamuzi ya Mkutano wa Kamati Kuu kuhusu kazi za uchumi na kuweka mkazo katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi na utulivu wa ajira na bei, ili kuuweka ufanisi wa uchumi ndani ya viwango vinavyofaa.

Hatua madhubuti zitachukuliwa ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa vifungu vya sera ya kuleta utulivu wa uchumi na hatua zake za ufuatiliaji. Miradi muhimu na uboreshaji wa vifaa na ukarabati unaoungwa mkono na zana za sera za fedha na bajeti zitaendelezwa ili kupata faida zaidi halisi.

Sera za kuongeza muda wa unafuu wa kodi ya nyongeza za thamani (VAT) kwa walipa kodi wadogo na mikopo jumuishi inayotolewa kwa biashara zenye ukubwa mdogo na wa kati zitatekelezwa kwa ufanisi.

Mkutano huo pia umesisitiza kwamba, ni muhimu kubaki na nia thabiti ya kuimarisha na kuendeleza uchumi wa umilikaji wa kiumma na kuhimiza, kusaidia na kuongoza maendeleo ya mashirika yasiyo ya umilikaji wa kiumma, kulinda haki halali na maslahi ya biashara za kibinafsi na kukuza soko lenye mwelekeo wa kimataifa, mazingira ya biashara yenye hadhi ya kimataifa yanayofuata mfumo mzuri wa kisheria. Pia uchumi wa kidijitali utasaidiwa katika kutafuta maendeleo endelevu na yenye uthabiti.

Mkutano huo umesisitiza haja ya kuwezesha ufunguaji upya wa haraka wa biashara na uzalishaji baada ya likizo ya Mwaka Mpya wa Jadi wa China na kutoa huduma nzuri kwa wafanyakazi wahamiaji wanaporejea kazini au kupata kazi mpya.

"Tunahitaji kuongeza juhudi za kutekeleza sera za kupanua matumizi," Waziri Mkuu Li alisema.



## HABARI KANDA KASKAZINI

### TANROADS, TARURA waagizwa kupanda miti kwenye barabara zao

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imeuagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kuwa na mpango kazi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupanda miti 12,000 kando ya kila barabara wanayoisimamia.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, amri hiyo inatokana na agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Akizungumza jana mjini hapo, Makongoro alisema baada ya nchi kukumbwa na ukame kwenye baadhi ya maeneo, ni vyema wakala hao na wananchi kutumia mvua inayoendelea kunyesha, kupanda miti ya kutosha kwenye maeneo mbalimbali na kwenye vyanzo vya maji.

"Pia ninaagiza halmashauri zote, taasisi za umma na binafsi, kupanda miti milioni 10.5 kwa mwaka mzima ili kutekeleza agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango la kutunza uoto wa asili," alisema.

Makongoro pia aliutaka Mtandao wa Vikundi vya Wakulima na Wafugaji Mkoa wa Manyara (MVIWAMA) kujitosa katika kampeni hiyo ya uhifadhi wa mazingira kwa kupanda miti 500,000.

Kutokana na agizo hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mati Super Brands Limited, David Mulokozi, alisema walishaanza kutunza mazingira kwa kupanda miti zaidi ya 15,000 na wanahitaji kuokoa ikolojia inayopotea ya Ziwa Babati.

"Mazingira ya Ziwa Babati yanahitaji utashi wa serikali na sekta binafsi kusaidia, kwa sababu magugu maji yamejaa na ziwa hili likikauka, hali ya hewa inaweza kuwa mbaya sana baadaye kama hatua za makusudi za kulihifadhi hazitaendelea kuchukuliwa," alisema Mulokozi.

Mratibu wa MVIWAMA, Valentin Ngorisa, alisema wameanzisha kampeni ya upandaji wa miti wilaya zote na mwaka huu watapanda miti 100,000.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema tayari wameshapanda miti 600,000 kwenye wilaya hiyo na kampeni inaendelea.

# Shughuli za kibinadamu zatishia baionuai msituni

**a Mary Mosha,** SAME

HIFADHI ya Mazingira Asili ya Msitu wa Chome ulioko Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro inatishiwa na ongezeko la shughuli za binadamu zinazoiweka hatarini baionuai yake kupotea.

Msitu huo asili wenye ukubwa wa hekta 14,283, unatambulika kitaifa na kimataifa kutokana na utajiri mkubwa ulionao katika baionuai na chanzo kikubwa cha maji kwenye maeneo ya Same na kwingineko.

Akizungumzia tishio hilo jana na kutoa hadhari kwa wanaoendelea kuhujumu hifadhi hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema uvumilivu wake una mwisho, hasa kwa mtu atakayekata au kuchoma misitu wakati ambao serikali na wadau wa mazingira wanapambana kuurejesha uoto wa asili.

Hifadhi Asili ya Chome inapata ufadhili wa Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) ambao hutoa mchango mkubwa wa fedha kwa ajili ya kufanya doria.

Majukumu mengine ni kukarabati njia za watalii ndani ya msitu, kutangaza msitu huo kwenye mitandao mbalimbali na kuwajengea uwezo wanakijiji wanaishi jirani na msitu ili kuanzisha miradi ya kuwaingizia kipato.

Kwa mujibu wa Babu, uoto asili wa msitu huo uko hatarini kutoweka kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu, hali ambayo imesababisha baadhi ya vyanzo vya maji kukauka na kutishia upatikanaji wa maji kwenye wilaya hiyo.

Mkuu wa Mkoa ameagiza Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kushirikiana na wananchi wanaozunguka hifadhi ya msitu huo kuulinda ili baionuai zisitoweke.

"Hii misitu inatakiwa itunzwe na kuhifadhiwa kwa sababu ndiyo uhai. Ikihifadhiwa vizuri, inasaidia vyanzo vyetu vya maji, ambavyo vinasaidia wananchi wetu walio maeneo ya chini kupata maji, sasa huku juu kuna tatizo ambalo lipo la watu kuchoma misitu ovyo na kwa makusudi kwa mambo wanayojua wao," alisema.

Kamanda Msaidizi wa TFS Kanda ya Kaskazini, Yusufu Kajia, alisema msitu huo unakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwamo ya uvamizi wa mipaka, uchimbaji wa madini, matukio ya uchomaji wa moto, uvunaji wa miti kwa ajili ya mbao na mazao ya misitu yasiyo ya mbao.

Emannuel Kiengi, Ofisa Maliasili mkoani hapa, alisema mradi wa EAMCEF umelenga kuisaidia serikali katika kutunza na kuhifadhi mazingira ya msitu wa Chome.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Mati Super Brands Ltd, David Mulokizi, akizungumza wakati wa uzinduzi wa upandaji miti 5,000 kuzunguka Ziwa Babati mwishoni mwa wiki. **PICHA: MARY MARGWE**

# TANROADS kuvibomoa vibanda vilivyojengwa kando ya barabara

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Arusha umetangaza kuanza rasmi operesheni yake ya kubomoa vibanda vilivyojengwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara kuu ya Arusha/Makuyuni ili kupisha upanuzi wa barabara hiyo.

Meneja wa TANROADS mkoani humo, Regnald Masawe, amesema jijini hapo kuwa wananchi waliovamia na kujenga vibanda ndani ya hifadhi ya barabara, ndiyo watakaoathirika kwa kuwa hawana uhalali na eneo hilo na wanapaswa kuondoka mara moja.

Massawe alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki na wananchi wa Kisongo wakati wa utekelezaji wa operesheni hiyo iliyoibua taharuki kwa wafanyabiashara wadogo wa Arusha.

"Tupo hapa kwa ajili ya kuondoa vibanda, wananchi wanapaswa kuelewa kwamba yeyote aliyejenga kibanda ndani ya eneo la mita 30 kutoka katikati ya barabara ametenda kosa na anapaswa kuchukuliwa hatua na leo tumeanza kuviondoa vibanda hivyo," alisema.

Alisema eneo la hifadhi ya barabara ni moja ya maeneo hatarishi kwa yeyote atakayekimbilia kulitumia kwa kuwa hatakuwa na uhakika wa maisha yake na mali zake hasa kunapotokea gari kuacha njia.

Alisema mpango wa serikali kwenye maeneo hayo ya hifadhi ya barabara ni pamoja na kujenga vituo vya magari nje ya barabara kuu ili kuepusha magari makubwa kuegeshwa barabarani na kusababisha msongamano.

"Sisi kama wakala wa barabara tumepanga kujenga stendi nje ya barabara kuu kwenye maeneo yenye uhitaji ili kurahisisha magari kushusha abiria na kupakia bila bughudha kwa watumiaji wengine wa barabara," alisisitiza.

Masawe alisisitiza yeyote anayefanya biashara kwenye barabara ya akiba, anavunja sheria kwa kuwa watu wanatakiwa kukaa umbali wa mita 30 kutoka katikati ya barabara.

Mbali na ujenzi wa kituo cha mabasi, maeneo hayo ya hifadhi ya barabara yatatumiwa na TANROADS kuotesha miti na kutengeneza barabara za watembea kwa miguu.

Baadhi ya wananchi kwenye eneo hilo la Kisongo ambao waliathiriwa na bomoabomoa hiyo, waliipongeza TANROADS kwa kuboresha miundombinu yake, lakini wakaomba wasiharibiwe mali zao na kuomba waongezwe muda wa kufanya biashara ndogo bila kuweka vibanda.

"Kwa kweli hivi vibanda havistahili kuwapo kando ya barabara kuu na mimi ninaunga mkono zoezi hilo ila ninaomba hawa wafanyabiashara hususani kinamama wanaouza mboga na matunda waachwe waendelee kuuza bila kuweka vibanda," alisema Charles Lobulu, mkazi wa Kisongo.

Akiwa Kisongo, Meneja huyo wa TANROADS alikubali ombi hilo na kutoa mwezi mmoja kwa wafanyabiashara hao wa mboga na matunda kuendelea kuuza bidhaa zao hadi mwishoni mwa mwezi huu.





# Mbunge apinga wajawazito kuongozana na wenza kliniki

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UTARATIBU uliowekwa na serikali katika vituo vya afya nchini wa kuwataka wajawazito kwenda kliniki kwa mara ya kwanza wakiwa na wenza wao umetajwa kusababisha baadhi yao kushindwa kuhudhuria kliniki kutokana na waume zao kugoma kuongozana nao.

Hatua hiyo imedaiwa inahatarisha usalama wa wanawake kutokana na kushindwa kujua maendeleo ya ukuaji wa mtoto akiwa tumboni na kuwapo kwa vifo vingi vya wajawazito na watoto hususani unapofika muda wa kujifungua.

Mbunge wa Jimbo la Kahama, Jumanne Kishimba, alibainisha hayo jana katika ziara ya Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel ya ukaguzi wa ubora wa utoaji wa huduma katika zahanati, vituo vya afya na hospitali alisema, Wasukuma hawana desturi ya kuongozana na wake zao hususan kliniki.

Alisema mila za kabila za Wasukuma zinakinzana na utaratibu wa kuongozana na wenza wao kliniki kujua maendeleo ya mtoto tumboni hali inayosababisha wengi kushindwa kuanza kliniki na kuiomba serikali kuangalia upya ili kutoa fursa kwa wajawazito kuhudhuria bila vikwazo hivyo.

"Ni mwiko mwanamume wa kabila la Kisukuma kutembea na mke wake wakiwa wameshikana mikono au kwenda naye katika maeneo ya umma kama vile hospitali hususan akiwa na mjamzito, tuiombe serikali ibadili utaratibu huu ambao unasababisha wanawake kushindwa kupata huduma za afya," alisema Kishimba.

Kadhalika, Kishimba aliomba serikali kuwaruhusu wajawazito kufika vituoni bila kuwa na wenza wao ili kuwanusuru na vifo vitokanavyo na uzazi wanapokwenda kujifungua, kwa kuwa ni muhimu mjamzito kuangaliwa ipasavyo kipindi chote cha ujauzito wake.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, alisema Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa siku wanaojifungua ni 45 hadi 60 wastani wa darasa moja na kwamba serikali inapaswa kuongezewa bajeti ya dawa na madaktari bingwa.

Alisema huduma za afya kwa mama na mtoto zimeboreshwa na serikali katika hospitali hiyo hali ambayo imewahamasisha wajawazito wengi kutoka maeneo mbalimbali kuja kujifungulia hospitali hii kwa siku wagonjwa wa nje (OPD) wanaohudumiwa ni 700 hadi 900.

Akijibu hoja hiyo Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Molel, alikiri kupokea malalamiko hayo na kuwaagiza waganga wakuu wa wilaya kuwatumia machifu katika maeneo hayo kutoa elimu hiyo ili wanaume waelewe utaratibu huo na kuongozana na wake zao siku za kliniki.

"Niwaagize waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuna mila zinazokinzana na utaratibu huu uliowekwa na serikali, tuwatumie machifu kwa kuwapatia elimu ili wajue umuhimu wa utaratibu huo ambao umewekwa na serikali, tusijikite kuwanyima huduma na badala yake tuwapatie elimu," alisisitiza Molel.




Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Benki ya TCB, Chichi Banda (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa mifuko 100 ya saruji kwa Diwani wa Kata ya Goweko, Shaban Katalambula, iliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha afya kwenye kata hiyo, hafla iliyofanyika Wilaya ya Uyui mkoani Tabora. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwenyekiti CCM ashauri wazazi kulinda watoto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Shinyanga Mjini, Anord Makombe, amewaomba viongozi pamoja na wazazi kuwalinda watoto wao dhidi ya vitendo vya ubakaji, ulawiti, kufundishwa ushoga pamoja na usagaji.

Makombe alitoa wito huo juzi wakati Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Shinyanga Mjini ilipoadhimisha miaka 46 ya kuzaliwa kwa CCM.

Alisema wazazi wanapaswa kuwapeleka watoto wao shule ili wakasome na kutimiza ndoto zao pamoja na kuwahakikishia usalama wao kwa kushirikiana na viongozi ili wasifanyiwe vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Nawaomba wazazi muwapeleke shule watoto wote ili wakasome na kupata elimu na kutimiza ndoto zao pia mshirikiane na viongozi kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, ikiwamo ubakaji, ulawiti kufundishwa ushoga na usagaji ili wasome na kutimiza ndoto zao," alisema Makombe.

Aidha, aliwaomba Watanzania kuendelea kukiamini chama hicho kutokana na kutekeleza ilani ya uchaguzi kwa vitendo na kuhakikisha miradi mbalimbali ya maendeleo inakamilika.

Naye Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Shinyanga Mjini, Rehema Nhimanilo, alisema katika maadhimisho hayo ya miaka 46 ya kuzaliwa kwa CCM, wameamua kutoa misaada mbalimbali kwa wahitaji, kikiwamo kituo cha kulea watoto wenye ulemavu na wanawake ambao wamejifungua kituo cha afya cha Kambarage.

Misaada waliyotoa ni pamoja na sabuni za kufulia na mafuta ya kujipaka, huku akitoa wito kwa wananchi na wadau wengine wa maendeleo kujitokeze kusaidia watoto hao wenye ulemavu ambao wanalelewa katika kituo cha Buhangija na kuwatatulia baadhi ya matatizo ambayo yanawakabili.

# DED aagiza wenyeviti vijiji/mitaa kushiriki vikao

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, amewaagiza wenyeviti wa serikali za vijiji na mitaa kushiriki katika vikao vya maamuzi kuhusu mpango wa kutoa chakula cha shule kwa wanafunzi na kusimamia utekelezaji ili kuondoa malalamiko kwa wazazi.

Alizishauri shule zenye maeneo makubwa kwa ajili ya kilimo cha mazao ya chakula ambayo yatasaidia wanafunzi kuwaondolea mzigo wazazi wa kuchangia vyakula na kwa kipindi hiki cha mabadiliko ya tabianchi wanaweza kulima yanayostahimili ukame kwa kuanzia.

Msumba aliyabainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya uwezo wa vyakula shuleni wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha manispaa hiyo cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023, alisema, kumekuwapo na malalamiko ya wazazi ya aina gani ya vyakula vinatakiwa kutolewa shuleni.

Aidha, alisema shule zote ni mali ya wananchi na wao ndiyo viongozi wanaowaongoza ni wajibu wao kushiriki vikao vya maamuzi ili kupunguza malalamiko ya wazazi kuhusu aina ya vyakula wanavyotakiwa kuchangia kwa ajili ya chakula cha mchana kwa wanafunzi wao.

Msumba alisema kuna baadhi ya shule zimekuwa zikitofautiana aina ya vyakula vinavyotolewa kwa wanafunzi hali ambayo imeibua malalamiko kwa wazazi kwa kuwa wengi wao wana kipato cha chini na kushindwa kumudu gharama za vyakula shuleni na kuagiza wenyeviti kusimamia suala hilo kwa kushirikiana na kamati za shule.

Mbunge wa Jimbo la Kahama, Jumanne Kishimba, alisema wilaya hiyo inalima mazao ya mahindi, mchele na maharage na kwamba kila shule inatakiwa kuchagua aina moja ya chakula ambacho kitatolewa na wazazi na sio kila mzazi atoe chakula anachoona yeye kinamfaa kwa mtoto wake.

Ofisa Elimu wa shule za msingi wilayani Kahama, Hamida Kaganda, alisema kabla ya kuainisha chakula gani kinachotakiwa kuliwa na wanafunzi wanapokuwa shuleni ni lazima kamati za shule zikae na kutoa maamuzi ya chakula gani kinatolewa kulingana na aina ya mazao yanayolimwa katika maeneo yao.

Alisema kufanyika kwa vikao kutasaidia kuondoa malalamiko ya wazazi na kwamba uchangiaji huo ni lazima na sio hiari.

Vile vile, wanafunzi wanapopata chakula shuleni inawasaidia kuongeza ufaulu na kudhibiti utoro.



## Ndivyo shule inavyoandaa wasomi jasiri, waibua fursa, wanaong'ara

Ukurasa 13



Ukurasa 12

## Mamia walivyonusuriwa na ujinga, umaskini hata njaa

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Bunge linaposhangazwa, kuhoji kozi Chuo Nyerere

•Ni udahili wa walimu wakati maelfu ni 'jobless' mitaani

KAMATI ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, inakitembelea Chuo Kikuu cha Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT).

Ni taasisi ya umma ya elimu ya juu iliyoanzishwa mwaka 2012 ikijengwa wilayani Butiama, mkoani Mara, ikilenga kuwa kitovu cha mabadiliko ya kilimo nchini.

MJNUAT miongoni mwa vyuo vikuu vinavyotarajiwa kuzalisha wataalamu wa kilimo na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), hivyo, inabainika kuwa kinataka kuweka kozi za ualimu, badala ya zile zenye mahitaji makubwa katika soko la ajira, hivyo kutakiwa kujielekeza katika kuanzisha kozi zinazoendana na usajili wa chuo hicho.

Huo ni ushauri wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii inapotembelea chuo hicho hivi karibuni na kubainisha kuwa serikali imepanga kudahili wanafunzi wa ualimu chuoni hapo ilihali wapo wahitimu wengi wa ualimu mitaani wasio na ajira.

Mjumbe wa kamati hiyo, Husna Sekiboko, anashauri malengo ya uanzishwaji wa chuo hicho ambayo yanagusa ndaki ya kilimo, shule za uhandisi na teknolojia, uhandisi na teknolojia ya nishati na madini, shule kuu ya TEHAMA na biashara, vizingatiwe.

"Serikali ijielekeze katika kuanzisha kozi zinazoendana na usajili wa chuo, inasikitisha kuona imepanga kudahili wanafunzi wa ualimu chuoni, ilhali wapo wahitimu wengi wa ualimu waliopo mitaani bila kuajiriwa," anasema Husna.



Mbunge wa Butiama, Jumanne Sagina (wa pili kushoto) na viongozi wengine wakiwa pamoja baada ya kumaliza kutembelea chuo hicho. **PICHA: MTANDAO**

Mjumbe huyo anahoji: "Hivi mnataka kuendelea kuzalisha walimu, ili muwafanyie nini? Hivi ni kweli kwamba hamjui kuwa kuna walimu maelfu waliohitimu kwenye vyuo vyetu hapa nchini wapo mitaani bila ajira?

Rose Tweve ambaye ni mjumbe wa kamati hiyo, anasema kama serikali inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuzalisha walimu, itumie vyuo vilivyoko ambavyo vina kozi hiyo badala ya kuendelea kuanzisha vyuo vipya.

"Utafiti gani mmefanya mkabaini kuwa hiki chuo pia kinatakiwa kuendelea kuzalisha walimu tofauti na vyuo vilivyoko? Anahoji Rose na kutoa ushauri kwamba wapelekwe Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaa (DUCE).

Anafafanua kuwa kama serikali inahitaji sana walimu, wawapeleke DUCE na kwingineko, ili kukiacha chuo kiendelee kozi za kilimo na teknolojia, kwa kuwa mahitaji ni makubwa na kuna fursa pia.

**WIZARA YAKUBALI**

Baada ya hoja hizo, Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, anasema serikali inazichukua hoja hizo na kwenda kuzifanyia kazi haraka iwezekanavyo.

Anafafanua kuwa chuo hicho kilichoanzishwa mwaka 2010 baada ya kuchukuliwa kwa majengo ya Shule ya Sekondari Oswald Mang'ombe, kinatarajia kwa mara ya kwanza kupokea wanafunzi Novemba mwaka huu.

"Chuo kimepata Shilingi bilioni 2.3, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, lakini kwa vile ujenzi utachukua miezi 18 tumeamua kutenga milioni 500 tufanye ukarabati hapa Oswald Mang'ombe, ili masomo yaanze wakati kazi zikiendelea ili kuchukua wanafunzi wengi zaidi," anasema.

Mbunge wa Butiama ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini, anaishauri Wizara ya Elimu kuangalia namna ambavyo itawezesha ujenzi wa chuo kuanza na kukamilika kwa wakati.

Anasema wana Butiama wamesubiri zaidi ya miaka 14, na kwamba, ingawa tayari kuna fedha, wananchi wanataka kuona kazi inafanyika haraka, ili chuo kiweze kuanza kazi haraka iwezekanavyo.

"Kwa kuwa hiki chuo hakina bodi ya manunuzi niiombe wizara kupeleka majukumu ya bodi hiyo katika ofisi ya mkuu wa mkoa ambako kuna wataalamu," anashauri Sagini.

Anaiambia wizara kuwa kuwapo kwa chuo hicho, wananchi, wakulima wa kawaida watakuwa na fursa ya kupata kozi fupi ambazo zitawasaidia kuboresha shughuli zao hasa za kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Mara Meja Jenerali Suleiman Mungiya, anasema chuo hicho kinachochea maendeleo na kuwataka wakazi wa mkoa huo kuchangamkia fursa za

INAENDELEA UK. 12

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Mamia walivyonusuriwa na ujinga, umaskini hata njaa

## Ni wanaoishi nyumba za matope na mbumbumbu



Wanafunzi wakiwa kwenye moja ya mchezo. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

MKOANI Dar es Salaam unapozungumzia Dial Community of Tanzania, watoto na jamii za kaya za wahitaji kutoka kata ya Kunduchi, wanafahamu umuhimu wa taasisi hiyo. Ni kwa sababu kuanzia mwaka 2013 imekuwa bega kwa bega na watoto wa kaya maskini kuwasaidia kupata elimu bora ya msingi na sekondari.

Ni shirika kutoka Korea Kusini, lililoanzishwa rasmi 2013 Kunduchi Mtongani, eneo la Skanska na kuanzisha mradi wa kutoa elimu kwa watoto hao baada ya kugundua kata hiyo ina watoto wengi wanaoishi katika mazingira magumu, hawasomi, wanakaa katika nyumba duni za udongo zinazobomoka wakati wa mvua.

James Aluthe, mwalimu wa Dial Community, anazungumza na Nipashe akisema hadi sasa wameanzisha darasa maalumu ili kufundisha watoto masomo ya shule za msingi mojawapo ni stadi za maisha.

"Tunafundisha watoto kuanzia miaka 8-13 waliokwama kwenda shuleni au wanaoishi katika mazingira magumu ambao wazazi wao hawakuwapeleka darasani kutokana na matatizo mbalimbali kama kushindwa kuwahamisha, kupelekwa bibi au babu hata kukosa fedha za kununua vifaa vya shule."

Anasema wanafundisha kusoma, kuandika na kuwaombea nafasi katika shule za msingi. Wanalenga kusaidia watoto wengi ili wafike chuo kikuu.

Aluthe anasema pia wanaoingia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) ili wafundishwe ndani ya mwaka mmoja kisha waendelee na darasa la nne na kupata nafasi ya kuendelea na darasa la tano na kumaliza.

"Sasa hivi kuna watoto wanaokwenda sekondari kupitia mfumo huu na wengine wapo msingi na kila mwaka 40 wanaingia shule ya msingi," anasema.

### CHAKULA SHULENI

Mwalimu Aluthe anasema shirika limeanzisha programu maalumu ya chai na chakula kwa wanafunzi kupunguza njaa na utoro kwa lengo la kufanikisha ufaulu na kwamba wameanzisha darasa la Hope Class ili kufundisha watoto michezo mbalimbali ukiwamo wa mpira wa miguu na riadha.

Aidha, Dial Community of Tanzania imejenga nyumba 40 kuhudumia watoto wanaoishi katika mazingira duni na hivi sasa watoto wanaishi vizuri na wakirudi nyumbani wanasoma katika mazingira bora badala ya kukaa ndani ya vyumba vya udongo ambavyo wakati wa mvua vilikuwa vinavuja.

"Tunaomba jamii nyingine au mashirika mengine yajitokeze kwa ajili ya kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu au wanaweza kutoa misaada kwa shirika hili na hatimaye shirika likawafikia wahitaji, wanaweza kusaidia mavazi, sare, daftari, viatu na hata kujengea kaya maskini nyumba," anasema Aluthe.

### SHINDANO LA VIPAJI

Ili kusaidia watoto kuonyesha vipaji vyao, hivi karibuni shirika linaandaa shindano kwa watoto kutoka kata ya Kunduchi. Aluthe anasema zaidi ya wanafunzi 200 kutoka shule za msingi na wengine walioko nje ya madarasani, nyumbani na mitaani nao walishiriki.

Hemed Hassan ni miongoni mwao mwanafunzi huyu, anayefurahia kushinda na kupata zawadi, akisema "Kwa kweli nilijisikia vizuri kwa sababu nilishiriki kuonyesha kipaji changu, nikashinda na hatimaye kupata zawadi ya toi ya treni."

Hemed anaibuka kidedea akiwa na kipaji cha kutengeneza gari na kuwataka wasioshinda wasikate tamaa, waendelee kujitahidi katika mashindano yanayokuja na huenda wakashinda. Mbali na hilo, anaishukuru Dail Community of Tanzania kwa kusaidia watoto wa kaya maskini kupata elimu, chakula na huduma za afya, mafunzo ya aina mbalimbali, sare, viatu na unga kila mwezi.

Akizungumzia shindano hilo, Mohamed Hamis kutoka familia maskini, anasema ni muhimu kutangaza vipaji vya watoto lakini pia linasaidia watoto kupewa zawadi mbalimbali pamoja na chakula kama mchele kilo mbili kwa sababu asilimia kubwa ya watoto walioshiriki katika shindano hilo ni wa familia zenye kipato duni.

### KAZI INAYOFANYIKA

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Dail Community of Tanzania, Inwook Park, anasema kila mwezi shirika hilo linatoa chakula, mafuta ya kupikia, nauli ya wanafunzi, gharama za matibabu, viatu vya shule, sare kwa watoto wanaotoka familia maskini.

Pia kuanzia mwezi ujao hadi Desemba shirika litaendelea kusimamia darasa la 'Hope Class' ili kusaidia watoto ambao hawakufanikiwa kwenda kusoma elimu ya msingi kutokana na matatizo ya kifamilia ikiwamo wale waliokosa uhamisho, waendelee kupata chakula shuleni ili wapate kusoma na kufundishwa bila vikwazo na kuongeza kuwa kila Jumamosi zaidi ya wato 900 wanapatiwa mikate kutoka shirika hilo.

Park anasema shirika limeanzisha programmu ya kufundisha wanafunzi wenye umri mkubwa kuoka mikate na ushonaji ili kuwapa ujuzi zaidi na pia wanafunzi wanafundishwa kompyuta na wanaingia maktaba kusoma vitabu vya aina mbalimbali.

# Bunge linaposhangazwa, kuhoji kozi Chuo Nyerere

INATOKA UK. 11

kuanzishwa kwake.

"Ninaamini chuo hiki kitachagiza maendeleo ya mkoa wetu, hivyo wito wangu kwa wananchi wa mkoa huu kuona hilo na kuanzisha miradi," anasema Meja Generali Manguya.

Anatoa wito huo wakati akiongoza warsha ya wadau alipokuwa akitambulisha mradi wa ujenzi wa chuo baada ya kupokea mkopo wa masharti nafuu Shilingi bilioni 102.3 kutoka Benki ya Dunia.

Warsha hiyo ilifanyika hivi karibuni mjini Musoma, huku akiwataka watendaji na viongozi wanaohusika katika ujenzi huo kuwa waadilifu, weledi ili mradi ukamilika kwa wakati.

"Viongozi katika maeneo mbalimbali waelimisheni wananchi kuhusu fursa zinazotokana na kuanzishwa kwa chuo hiki ikiwamo kuongezeka kwa nafasi za mafunzo ya elimu ya juu, ili nao waweze kuchukua hatua za makusudi kuboresha shughuli mbalimbali," anasema.

Katika warsha hiyo, Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Lesakit Mellau anataja lengo la serikali kuanzisha MJNUAT ni kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

"Tayari chuo kimeandika miradi mbalimbali na ikifadhiliwa yote, kitakuwa na miundombinu ya kutosha, ili kudahili wanafunzi 15,000 katika kampasi mbalimbali za mkoa wa Mara na Tabora," Profesa Mellau anasema.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Fedha, Mipango na Utawala Profesa Msafiri Jackson, anasema ujenzi chuo unahusisha ndaki ya kilimo na shule kadhaa zikiwamo za uhandisi na teknolojia, nishati na madini na TEHAMA.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ndivyo shule inavyoandaa wasomi jasiri, waibua fursa, wanaong'ara

KATIKA jitihada za kuwaandaa vijana walioko shuleni ili baada ya kuhitimu wakabiliane na mahitaji na changamoto za dunia ya leo, Sekondari ya Imperial iliyoko Msolwa Chalinze mkoani Pwani, inawatayarisha wanafunzi kuwa majasiri na wenye uthubutu kupitia kampeni ya Be Bold Go Bold, inayowahakikishia kuishi na kumudu maisha bila kutetereka.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mwalimu Mkuu wa Taaluma, Rogers Lutambi, anasema

"Be bold Go Bold inakwenda kuwapa wanafunzi wao muunganisho wa vile wanavyosoma shuleni na kile kilichoko mtaani au dunia wanapoishi, kwa kuhamasisha ubunifu zaidi.

Anasema vijana wengi wamekuwa wakilalamikiwa kuwa pamoja na elimu wanayopata hawaajiriki kutokana na uwezo mdogo tofauti na vyeti vyao, lakini ukosefu wa ajira na changamoto nyingine nyingi zilizoko mtaani zimesababisha ukosefu wa uwiano wa kile kinachofundishwa na kile wanachokutana nacho mtaani.

"Katika nyakati zenye changamoto huja uwezo wa kuona na kuchukua fursa za kuchangamkia katika karne hii ya 21, Imperial tunalenga kuchochea ubunifu utakaoleta tija kwa wanafunzi wetu wanaomaliza shule na hatimaye kujiunga na kampuni na taasisi mbalimbali au kujiajiri wakiwa wenye uwezo wa kuendana na karne hii."

Mwalimu Lutambi anaongeza: "Tumetiwa moyo na ujasiri wa wanafunzi wetu wenye vipaji, wafanyikazi na walezi, ambao wanafanya kazi ili kujitofautisha na kuendeleza shule yetu kama kiongozi katika elimu ya nadharia. Kampeni ya Be Bold Go Bold inaahidi kuendeleza juhudi zetu hizi na kutumika kama njia kuelekea uwezekano mkubwa zaidi wa kupata vijana wenye uwezo wa waohitajika sokoni."

"Imperial, tunaamini kwamba vipaji vinastahili kupewa nafasi na fursa, inamaanisha kutoa uzoefu wa kipekee na tofauti ndani na nje ya darasa ambao huwezesha mafanikio na ustawi wao. Na inamaanisha kukuza kikundi chetu cha wanafunzi kimkakati ili kuhakikisha kuwa wanafunzi zaidi wanaweza kushiriki kikamilifu na wanaomaliza na uzoefu wa kujifunza Kwa vitendo ili kuleta mabadiliko.

Dunia ya sasa inahitaji watu walio majasiri katika kufikiri au kijasiri katika utendaji na ujasiri katika kujitambua na kwamba kupitia kampeni hiyo, tutahakikisha kwamba kila mwanafunzi wa Imperial, anapata anwani kamili ya fursa za kujifunza ambazo zitawawezesha kufikia ubora na kuleta matokeo katika maisha yao yote, lakini tutawapatia walimu rasilimali za kutosha za ufundishaji bora, kama ngao ya mkakati huu.



Wanafunzi hawa kupitia programu ya Go Be Bold wanaandaliwa kuwa tofauti kuanzia ujasiri, uadilifu, ubunifu hadi kuona na kutumia fursa shuleni na mitaani wanakoishi. **PICHA: IMPERIAL.**

**KUINUA VIPAJI**

Mwalimu wa taaluma, anaongeza kuwa wamejipanga kuunganisha dunia ya nje inavyokwenda na kile tunachofundisha darasani na wataendeleza uchunguzi unaoendeshwa na udadisi na kusaidia ugunduzi kati ya wanafunzi na waelimishaji wao wanaotazamiwa kuwa kama chachu ya kupeleka vijana wenye uwezo mtaani.

Vijana ambao watachunguza masuala makubwa zaidi ya wakati huu na kutatua changamoto muhimu zaidi na kwamba mpango huo utawawezesha wanafunzi kubadilisha mawazo kuwa vitendo na kuhakikisha maendeleo ya kweli katika usalama wa mtandao, kuzuia magonjwa, kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi. Kwa jumla, watafuata kwa ujasiri njia mpya kwa jamii zenye nguvu, mazingira bora na maisha bora, anaongeza.



Akizungumza kukuza ubunifu anasema ni kiini cha hekima isiyo ya kawaida na kwamba kutawapa wanafunzi nafasi na kujifunza na kukuza ubunifu na kujipanga kuwa kitivo cha vijana wabunifu kwa kuangalia kila fursa ya kufikiria nje ya mipaka na kuwajenga kuwa imara kuangalia mazingira ya kuhatarisha kwa umakini na kuwa macho katika kufuata yasiyojulikana, kuchimba zaidi na kutafuta miunganisho na kukumbatia mawazo yao, kama wasanii na wavumbuzi.

Kupitia Be Bold GO Bold, waanamini watazalisha enzi mpya ya michango ya ubunifu kwa kuimarisha kujitolea kwa sanaa na kuibua uhusiano mpya kati ya taaluma ikijumuisha upanuzi mkubwa wa jengo la sanaa, kwa kuuimarisha uhusiano wa wahitimu au alumni na kukuza juhudi za kuongeza ushirikishwaji katika sanaa katika maisha baada ya shule, anaongeza Lutambi.

**KUANDAA VIONGOZI**

Mwalimu Lutambi anasema, hitaji la viongozi wenye maadili na wabunifu liko wazi zama hizi na kuongeza:

"Tutashirikiana na wanafunzi waliopita katika kufikiria upya mazingira yetu yaliyojengwa, na kuwatengeneza vijana wenye uwezo wa kukabiliana na maswali makubwa katika siasa na mawazo ya kijamii huko nje. Tunatazamia kuwajenga vijana kuwa wenye maono. Wakati tofauti za kiafya na kiuchumi zikiongezeka, mizozo ya kijiografia na kisiasa ikizidi kuongezeka na kubadilika kila mara."

"Aidha, teknolojia zinazoibuka na machafuko ya kijamii vikitusukuma kuvuka mipaka mipya ya kimaadili, hitaji la viongozi wenye maadili na wabunifu liko wazi. Tunahitaji watu mahiri, wenye nia ya ujasiriamali ambao wana ujasiri wa kuleta matokeo na uadilifu wa kufanya kile kilicho bora na sawa, hasa katika kipindi hiki kigumu."

Anasema mkakati huo umelenga kuwapa wanafunzi ukakamavu wa kitaaluma, wenye kutia moyo, fursa za kuona na kujifunza kuhusu maisha na mazingira ya kujifunzia ambayo yanaanzia hapo shuleni na kuenea duniani kote.

**KURITHISHA UZOEFU**

Lutambi anaeleza kuwa wataunda madaraja ya kujifunza kupitia kwa watu waliofanikiwa na kwa njia ya kampeni hiyo waaamini katika kupeleka mtaani vijana wataongoza kampuni na timu za matibabu na wataandika muziki na katiba za demokrasia mpya hapo baadaye.

ELIMU
## NA SABATO KASIKA

# Wanakijiji wanaposema imetosha sasa, wajichangisha kujenga sekondari ya kijiji

•Kero umbali mrefu sekondari kata, mrundikano, uhaba vyoo



Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Halfan Haule (mwenye kofia), akishiriki katika ufyatuaji wa matofali ya ujenzi wa Shule ya Muhoji Sekondari.

KUCHOSHWA na tabu wanayoipata watoto wanaotembea kilometa nyingi kila siku kuwahi shuleni, mrundikano wa wanafunzi darasani, utoro na kukimbia kusoma kutokana na kuchoka, badala ya kufurahia masomo, kumewachochea wazazi na walezi kujichangisha na kujenga sekondari ya kijiji.

Licha ya kukiri kuwa kuna sekondari ya kata kilipo kijiji chao na kushukuru kuwa shule za kata zilizo karibu kila mahali nchini, zimewanufaisha wanafunzi wengi kupata elimu katika maeneo jirani, changamoto zinazozikabili zimekuwa pia mtihani mkubwa kwa watoto wao.

Ari ya kutaka kujenga shule ya kijiji imeibuka katika kata ya Bugwema iliyoko Wilaya ya Musoma mkoani Mara, inayoundwa na vijiji kadhaa kikiwamo cha Muhoji.

Wazazi na walezi wa kijiji hicho wamechoshwa na watoto wao kutembea kilometa zaidi ya 18 kila siku na kujichanga sasa wanajenga sekondari ya Muhoji.

Wanakiri kuwa wanachukua hatua hiyo, baada ya kuona mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji si rafiki kwa wanafunzi na walimu katika sekondari ya kata ya Bugwema kutokana na umbali mrefu.

Licha ya kuwapo na vijiji vingine vya Masinono, Kinyang'erere na Bugwema vinavyounda kata hiyo, wana Muhoji wamejitolea kujenga sekondari ya kijiji hicho, ili kuwapunguzia watoto wao usumbufu wa umbali wa kwenda shule na kurudi nyumbani.

Mtendaji wa kijiji hicho, Samwel Maurice, anasema wiki iliyopita ilifanyika harambee ya kuchangia ujenzi wa sekondari hiyo, huku wakazi hao, wakiwa wamechangia mifuko 124 ya sementi Shilingi 305,000.

Anaiambia Nipashe: "Harambee hiyo imefanyika wiki iliyopita Januari 24 ikisimamiwa na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo na kupatikana mifuko hiyo na kiasi hicho cha fedha ambavyo ni mbali na nguvukazi."

Anafafanua kuwa wananchi wanaendelea kutoa michango yao ikiwamo nguvukazi kwa kusomba maji, mawe, mchanga na kokoto na kwamba kijiji kina kaya 449 ambapo kila kaya inatakiwa kuchangia Shilingi 45,000.

"Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Halfan Haule, naye amechangia mifuko 20 ya saruji na kushiriki katika ufyatuaji wa matofali. Profesa Muhongo ametoa mifuko 150 na ameahidi kuendelea izaidi," anasema.

### KUANZA MWAKANI

Mtendaji huyo anasema, wananchi wamejiwekea malengo ya kujenga vyumba vinne vya madarasa, ofisi mbili za walimu na matundu nane ya vyoo, ambavyo vyote wanatakiwa vikamilike kabla ya Julai 30, mwaka huu.

"Tunatamani Muhoji Sekondari ifunguliwe Januari 2024, hivyo tunakaribisha michango kutoka kwa wadau wa elimu, ili kufanikisha kile tulichokikusudia, kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya watoto wetu," anasema Maurice.

Mratibu Elimu Kata, Abdalah Ukwaju, anasifu hatua iliyochukuliwa na wakazi wa kijiji hicho ni ya kuigwa, kwa kuwa inalenga kuboresha elimu kuanzia mazingira ya kujifunzia na ufundishaji.

"Hatua yao hii inaunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu kwa kuhakikisha kila mtoto anaipata katika mazingira ya karibu, hivyo niwapongeze kwa kujenga sekondari ya kijiji chao," Ukwaju.

Ukwaju anawaomba wadau wa elimu wa Kata ya Bugwema kuungana na wakazi wa kijiji hicho, kwa kutoa mchango, ili kufanikisha ujenzi huo, na kwamba ikiwezekana, wanafunzi waanze masomo mwakani.

Mbunge Prof. Muhongo, anasema elimu ni uchumi na pia elimu ni maendeleo, huku akikaribisha watu wa kada mbalimbali kuchangia ujenzi wa shule za sekondari za vijiji katika jimbo hilo.

Anasema Musoma Vijijini ina vijiji 68 na kata 21, na kwamba baadhi ya kata ikiwamo za Nyakatende, kwa sasa zina sekondari zaidi ya moja ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi, serikali na wadau wengine wa elimu.

"Elimu ni uchumi, ni maendeleo, tushirikiane na wananchi na serikali kuongeza shule za sekondari, ili kuwapunguzia watoto wetu mrundikano madarasani na hata kutembea umbali mrefu," Profesa Muhongo anasema.

### BUGWEMA YAZIDIWA

Mkuu wa Sekondari ya Bugwema, Joseph Ndaro, anasema shule ina wanafunzi 742, madarasa 20, walimu 10, vyoo matundu sita ya wavulana na saba ya wasichana na nyumba tatu za walimu.

"Hayo madarasa 20 yanatosha kwa wanafunzi wote, ila changamoto ni hiyo ya idadi ndogo ya walimu, nyumba, matundu ya vyoo, lakini uhaba wa zaidi ya viti 300 vya wanafunzi," anasema Ndaro.

Anaongeza kuwa kama zilivyo changamoto za shule za sekondari za kata katika maeneo mengine, kadhalika Bugwema nayo na kwamba anaamini kuwa zinaendelea kushughulikiwa na serikali.

Anafafanua kuwa shule hiyo ilianzishwa mwaka 2006 na umbali mrefu ndiyo unaosababisha wananchi kuamua kujenga sekondari za vijiji vyao, ili kuwapunguzia watoto adha ya kutembea na kuchoka kila siku.

"Kwa mfano kutoka Muhoji hadi hapa Bugwema, ni kilometa tisa, hivyo ni wazi watoto wanachoka na kama kusingekuwa na changaamoto hiyo, Bugwema bado ina madarasa ya kutosha ya kuwachukua wanafunzi wote," anasema.

Aidha, anaongeza kuwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza Bugwema Sekondari mwaka huu ni 362, huku wa kiume wakiwa ni 202 na wa kike 160.

"Hata hivyo, walioripoti shuleni ni wanafunzi 227, wa wavulana 122 na wasichana 105. Tumeotoa taarifa kwa uongozi wa serikali katika kata yetu msako unaendelea, ili kuwapata wale ambao hawajaripoti," anasema.

Ndaro anasema shule inawapokea hata wale wasio na sare na kufafanua kuwa wapo baadhi ya wanafunzi wa kike na kiume, ambao wametamka wazi kuwa hawataki shule na kwamba taratibu za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.



Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (kulia), akihamasisha ujenzi wa shule hiyo.
**PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**





# LATRA yatakiwa kutekeleza majukumu kwa weledi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewaagiza wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia weledi na kuepuka vitendo vya rushwa.

Aidha, amewaagiza kuchukua hatua dhidi ya madereva na wasafirishaji wanaokiuka sheria za matumizi sahihi ya miundombinu ya usafirishaji na kusababisha ajali.

Senyamule, alisema hayo juzi katika hafla ya uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi wa LATRA jijini hapo.

Senyamule alisisitiza serikali kupitia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imewekeza fedha nyingi katika maendeleo ya miundombinu ya barabara na reli nchini.

"Hata hivyo, kuna baadhi ya madereva na wasafirishaji wanashindwa kutimiza wajibu wao na kusababisha maafa na taharuki kwa watumiaji wengine wa miundombinu hiyo," alisema.

Alisema mazingira ya wafanyakazi wa LATRA yanavishawishi vingi kutokana na mgongano wa maslahi ya watoa huduma mbalimbali na wanapaswa kufanya kazi kwa weledi na uadilifu ili kuboresha huduma inayotolewa kwa wananchi na kuepusha migogoro.

"Sisi Dodoma tumebahatika kupata miundombinu mizuri ya usafiri wa barabara na reli, LATRA mwendelee kutoa elimu ya matumizi sahihi ya miundombinu kwa umakini na kwa kufuata taratibu sahihi ili kukamilisha azma ya serikali ya kuwezesha maisha bora kwa Watanzania," alisema.

Alitoa rai kwa Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji (COTWU) kuleta mshikamano wa wafanyakazi na kushirikiana na menejimenti ili kuongeza tija na kuepusha migogoro mahala pa kazi.

"Baraza la Wafanyakazi ndiyo jukwaa la kisheria la majadiliano ya pamoja kati ya viongozi wa taasisi na wafanyakazi. Uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi ni agizo la mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la mwaka 1970 na ni utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004," alisema.

Mkurugenzi wa LATRA, Habibu Suluo, alisema baraza hilo jipya mkataba wake ulisainiwa Desemba 2022 na kuridhiwa Januari 2023.

Aidha, alisema mamlaka hiyo imepewa jukumu la kudhibiti usafiri wa reli, barabara na waya huku upande wa reli wakidhibiti Kati na TAZARA.

Vile vile, alisema shughuli nyingine wanazopfanya ni kudhibiti usafiri wa umma kwa abiria, malori na wanatekeleza majukumu yao yote kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizoko.



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godrin Mollel, akizindua kwa kukata utepe gari la kubebea wagonjwa lililotolewa na serikali kwa ajili ya kuhudumia Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## JOWUTA yaomba maslahi ya wanahabari yaangaliwe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi cha Waandishi wa Habari nchini (JOWUTA), kimeomba kamati iliyoteuliwa kuchunguza maslahi ya wanahabari kuanzia ngazi ya chini ili ipate kile kilichokusudiwa na serikali.

Mwenyekiti wa JOWUTA, Claudia Gwandu, aliyasema hayo katika mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika jijini hapo na mkutano mkuu wa uchaguzi.

Alisema kamati ilioteuliwa na Waziri wa Habari na Teknolojia ya Mawasiliano, Nape Nnauye, inapaswa kuwasilisha hoja za msingi ambazo zitakwenda kuinua sekta ya habari pamoja na wanahabari wenyewe.

Alisema wasifanye suala hilo kwa ajili ya manufaa yao bali kwa ajili ya maslahi ya taaluma ya wanahabari wote nchini.

"Tunaomba kamati iende ikatende haki kwenye kazi waliyokabidhiwa tunahitaji kuona wanahabari wananufaika na sekta yao," alisema Gwandu.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Habari (MAELEZO), Rodney Thadeus, alisema angependa kuona chama hicho kinafanya kazi kwa weledi ya kuinua sekta ya habari juu kutokana na umuhimu wake kwa jamii.

Alisema chama hicho kinapaswa kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kuelimisha jamii pamoja na wao kufanya mambo ya msingi ambayo yanajenga taaluma.

Aliwataka viongozi waliochaguliwa wakawe chachu ya maendeleo badala ya kujinufaisha wenyewe.

Alisema serikali imewaamini na wao wanapaswa kuonyesha imani hiyo mbele ya jamii inayowazunguka kwa kuja na matokeo chanya katika uchunguzi wao.

Alisema muda waliopewa unatosha kubaini matatizo yaliyoko ndani ya tasnia ya habari nao watumie muda huo kuhakikisha wanafanya kazi hiyo kwa weledi.

# Wakuu wa idara waagizwa kusimamia miradi

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MKUU wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, amewataka wakuu wa idara mbalimbali za wilaya hiyo kuongeza nguvu katika kusimamia miradi mbalimbali ikiwamo ukusanyaji wa mapato kwa masilahi ya maendeleo ya wananchi.

Msuya, alisema hayo alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha madiwani wakiwamo wasimamizi wa idara mbalimbali kilichofanyika wilayani hapo.

Alisema wakiwa wasimamizi wakuu kwenye idara mbalimbali wanatakiwa kuongeza nguvu ya kusimamia miradi pia wakihakikisha wanakusanya mapato.

Alisema bado kuna baadhi ya wasimamizi wa idara ambazo zinasuasua na kushindwa kujisimamia wenyewe kwenye maeneo yao hali ambayo imesababisha kushindwa kufikia malengo kwa wakati kwa faida ya wananchi na kwa serikali pia.

Mkuu huyo wa wilaya pia aliwataka watendaji hao kuhakikisha kwenye maeneo yao hakuna mtoto yoyote aliyeandikishwa kuanza elimu ya msingi na yule ambaye amefaulu anakaa nyumbani kwa kisingizio cha kukosa sare ya shule.

Alisema kuwa watoto hao kama hawana sare za shule ni vizuri waende hivyo hivyo wakasome badala ya kuendelea kuwaweka nyumbani na wenzao wakiendelea na masomo. "Nasema kwenu nyinyi watendaji, madiwani na wazazi na walezi, watoto hao wanaostahili kuanza elimu ya msingi na wengine wa sekondari, wahakikishe wote hao wanaenda shule hata kama hawana sare za shule badala ya kuwaweka majumbani.

"Kwa umoja wenu mshirikiane katika suala hilo ni imani yangu ndani ya wilaya hii hakuna mtoto atakayebaki nyumbani kwa kizingizio cha kukosa sare ya shule kwa kuwa wote watakuwa wameandaa," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wakulima wa wilaya hiyo kutumia mvua inayonyesha kwenye kilimo ili waende sambamba kulinga na msimu ulivyo kwa mikoa ya kanda ya kati.



# Polisi yakamata shehena ya vipodozi vyenye sumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani hapo limekamata shehena ya vitenge na vipodozi vyenye viambata vya sumu vilivyopigwa marufuku nchini vikiingizwa nchini kwa njia za magendo.

Shehena hiyo ilikamatwa juzi wilayani Mbeya ikiingizwa kwa kutumia gari dogo aina ya Toyota Mark X lenye namba za usajili T. 948 ASL ambalo pia linashikiliwa na polisi.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema baada ya gari hilo kukamatwa dereva alikimbia na kulitelekeza.

"Tulipolipekua gari hilo lenye rangi ya silver, tulikuta kuna shehena ya vitenge zaidi ya jozi 79 sawa na doti 474 pamoja na vipodozi vya aina mbalimbali vikiwa ndani ya gari hilo," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema gari hilo linashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi ili kumbaini mmiliki wake pamoja na dereva aliyekuwa akiliendesha ili akamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo litaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha wanakomesha biashara ya magendo kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanafanya biashara kwa njia sahihi na zenye ushindani wa haki ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya serikali kwa usahihi.

Katika tukio lingine Kamanda Kuzaga alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kuanzisha na kuendesha kiwanda bubu cha kutengeneza vinywaji vikali vya aina mbalimbali.

Akifafanua tukio hilo, Kamanda Kuzaga alisema watu hao walikamatwa ndani ya nyumba moja ya makazi iliyoko Mtaa wa Ituha jijini Mbeya wakiwa wameanzisha kiwanda hicho ndani ya nyumba hiyo.


Aliwataja watu hao kuwa ni Yusufu George (38), mkazi wa Ituha na Frank David Kaseke (34), mkazi wa Gombe Kaskazini, Kata ya Itezi.

Alisema baada ya upekuzi ndani ya nyumba hiyo, watu hao walikutwa wakiwa na mtambo wa kutengeneza pombe hiyo, chupa nyingi za pombe za aina mbalimbali, nembo za vinywaji vya aina mbalimbali pamoja na vizibo vya chupa hizo.

"Pia tuliwakuta na katoni kadhaa ambazo walikuwa tayari wameweka pombe hiyo tayari kwa ajili ya kwenda kuiuza mitaani," alisema Kamanda Kuzaga.

Alitoa wito kwa wananchi hasa watumiaji wa vinywaji vikali kuwa makini na pombe wanazokunywa ili kuepuka zilizotengenezwa mitaani bila kuthibitishwa na mamlaka husika kwa vile zinaweza kuwaletea madhara ya kiafya.

Kamanda Kuzaga alisema watu hao watafikishwa mahakamani wakati wowote baada ya uchunguzi wa kina unaofanywa na polisi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za kiserikali kukamilika.



Jaffar Haniu akiapa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Rungwe jana katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ikiwa ni siku chache baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Viongozi CCM watakiwa kulinda mali za chama

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

VIONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika wilaya zote za Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kulinda mali za chama kwa kuhakikisha wanazitambua na zinawanufaisha wanachama wote.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wilayani Kyela wakati wa uzinduzi wa mbio za bendera za chama hicho ambazo zinalenga kuhamasisha utunzaji wa miradi.

Aliwataka kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na chama hicho ili kuhakikisha kinakuwa na wanachama wengi ambao watakisaidia kuendelea kushinda kwenye chaguzi mbalimbali zitakazokuwa zinafanyika.

"Uhai wa chama chetu unategemea uwapo wa wanachama wengi, kwa sasa tunaendelea kusajili wanachama kwenye mfumo wa TEHAMA, kwa hiyo mnapoendelea na usajili huo hakikisheni mnatafuta na wanachama wapya," alisema Dk. Mwakajumilo.

Aliwataka pia viongozi wa chama hicho kuendelea kutangaza vizuri miradi inayotekelezwa na serikali kwenye maeneo yao ili wananchi waendelee kuiamini serikali yao pamoja na chama.

Vilevile alizitaka kamati za siasa za wilaya kukagua miradi inayotekelezwa na serikali kwenye wilaya zao ili kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa.

**Aliwataka pia viongozi wa chama hicho kuendelea kutangaza vizuri miradi inayotekelezwa na serikali kwenye maeneo yao ili wananchi waendelee kuiamini serikali yao pamoja na chama.**

# Zaidi ya miti milioni 10 kupandwa kuhifadhi mazingira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya unatarajiwa kupanda miti milioni 10.5 mwaka huu kwa lengo la kuhifadhi mazingira, vyanzo vya maji na kurejesha uoto wa asili kwenye maeneo yaliyoharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu.

Kaimu Ofisa Mazingira wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Samora Mshang'a, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa upandaji wa miti kimkoa na kuwa kila wilaya imepangiwa idadi ya miti itakayopandwa.

Alisema miti itakayopandwa ni ya matunda, kivuli na mingine itapandwa kwenye vyanzo vya maji hasa ile ambayo ni rafiki wa maeneo hayo.

Alisema imezalishwa na taasisi mbalimbali zikiwamo halmashauri zote, watu binafsi na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na wilaya.

"Lengo letu ni kuhakikisha Mbeya inaendelea kuwa ya kijani kama ilivyo sifa yake, kwa hiyo tumeweka utaratibu wa kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 na wanatakiwa washirikiane na wataalamu kwenye upandaji wa miti hiyo," alisema Dk. Mshang'a.

Alisema baadhi ya miti hiyo itapandwa kwenye maeneo ya taasisi zikiwamo shule za msingi na sekondari zote na kwamba hata wanafunzi watashiriki kwenye upandaji huo.

Dk. Mchang'a aliwataka wananchi wa mkoa huo pia kushiriki kupanda miti hiyo kwa kuhakikisha kila mmoja anapanda nyumbani kwake hasa miti ya kivuli, matunda na kuni kwa ajili ya kulinda mazingira ya nyumbani kwao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka maofisa mazingira wa halmashauri kuhakikisha wanashirikiana na maofisa maliasili kusimamia upandaji wa miti hiyo ili kufikia lengo na halmashauri ambayo haitafikia lengo viongozi wake watachukuliwa hatua.

Aliwataka kuhakikisha miti hiyo inatunzwa ili isife na ilete matokeo chanya kuepusha kuwa na takwimu hewa za miti iliyopandwa na mazingira yanaendelea kuwa salama.

Homera aliwataka wananchi wa mkoa huo kuepuka kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji na kwenye misitu ya hifadhi ili kuhakikisha mazingira hayo yanaendelea kuwa salama.

Alisema vyanzo vya maji vinavyohifadhiwa ni kwa ajili ya faida ya wananchi wenyewe kutokana na vyanzo hivyo kutumika kwenye shughuli za kilimo, ufugaji, matumizi ya nyumbani pamoja na kutumika kwenye uzalishaji wa nishati ya umeme.

"Maeneo yote oevu yaendelee kuwa salama, sasa hivi tunaendelea kupambana na Bonde la Ihefu ambalo lilikuwa limevamiwa na wafugaji, nawaomba wananchi wote tushiriki kwenye utunzaji wa maeneo haya yana faida kubwa sana kwetu," alisema Homera.

Baadhi ya viongozi wa mila waliiomba serikali iwashirikishe kwenye ulinzi wa misitu wakieleza kuwa wanaishi na wananchi kwenye maeneo yao na wanaiheshimu misitu wanayoihifadhi wao.

Chifu wa Mkoa wa Mbeya, Rocket Mwashinga, alisema ipo misitu inayotunzwa na machifu na haivamiwi na wananchi na hata serikali wakishirikishwa itakuwa salama kuliko ilivyo sasa.

Alisema wana mbinu zao za kimila za kuilinda na uwezo wa kuzitumia mbinu hizo kulinda misitu ya serikali na kuwa salama.



## Waziri amulika ufanisi miradi ya TASAF Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utwala Bora, Jenista Mhagama, amesema wataendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha wananchi wasiojiweza kiuchumi, wanasaidiwa kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Alibainisha hayo jana alipozungumza na walengwa wa mpango huo kwenye Shehia ya Kianga wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya TASAF inayotekelezwa Zanzibar.

Jenista alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais Dk. Mwinyi wanafanya kazi kubwa kwa kutumia njia mbalimbali ili kuona Tanzania inaendelea kuwa na maendeleo yanayowafikia wananchi wote.

Alisema viongozi hao wanafanya kazi kubwa kupitia miradi, ukiwamo wa TASAF, kwa lengo la kuwanufaisha wananchi na kuwawezesha kiuchumi.

"Taifa linaendelea kusonga mbele na mabadiliko makubwa yanayonekana katika sekta mbalimbali ikiwamo utalii.

"Kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour, viongozi hao walijitoa wenyewe kufungua utalii na matokeo yake yanaonekana," alisema Jenista.

Aliwataka wanakaya kuendelea kuwahamasisha watoto wanaotokana na kaya zao kuhudhuria vizuri kwenye masomo yao kwa ngazi zote kuanzia maandalizi na msingi kwa kuhakikisha wanakwenda shuleni.

Hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kuwaunga mkono viongozi hao kwa kuwa wanafanya kazi kwa bidii katika kuleta maendeleo ya taifa.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu wa Baraza la Wawakilishi, Salhina Mwita, alisema serikali zote mbili zinafanya kazi kutokana na muungano uliopo ambapo miradi mbalimbali inatekelezwa kwa ushirikiano ukiwamo wa TASAF.

Mwakilishi wa Mwera, Mihayo Juma N'hunga, alisema ataendelea kushirikiana na serikali kusimamia miradi inayoanzishwa jimboni. "Hatuna budi kuungana na serikali yetu inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwani wananchi wamekuwa wakifaidika na jitihada hizo, wamekuwa na miradi mbalimbali," alisema.

Aliitaka serikali kuwajengea hospitali ili kusogeza huduma za afya, hasa za mama na mtoto ili kinamama wa Kianga na maeneo ya jirani wapate huduma ya kujifungua kwenye kituo kilichoko jirani na makazi yao.

Akisoma risala kwa niaba ya wakazi wa Shehia ya Kianga, Nuru Abubakari Mohammed alisema kupitia mpango huo wameanzisha vikundi mbalimbali vya wajasiriamali ambavyo vinaendelea kuwasaidia katika kujikimu kimaisha.

# Teknolojia mpya kunasa wahalifu kwenye misitu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Mkuu wa Idara ya Misitu, Miza Suleiman Khamis, amesema teknolojia ya ufuatiliaji kwa njia ya kamera (camera trapping) katika hifadhi za misitu itasaidia kulinda na kusimamia hifadhi za misitu na kuwanasa wahalifu.

Amesema hatua hiyo itasaidia kuwadhibiti watu hao wanaorudisha nyuma maendeleo nchini pamoja na kutambua aina za wanyamapori waliopo kwenye misitu hiyo.

Aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya mfumo wa usimamiaji wa maeneo ya ramani za jamii na usimamizi wa misitu (Tacare) yaliyoshirikisha wataalamu kutoka taasisi mbalimbali yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Chuo cha Utalii Maruhubi, Unguja.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kutoa taaluma kwa wataalamu hao kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia ambayo yatasaidia kuwanasa wahalifu na kupunguza vyanzo vya moto unaotokea kwenye hifadhi hizo.

Alisema matumizi ya teknolojia ya GIS (Geographic Information System) yanahitajika, hasa kwa wananchi wa vijiji vilivyouzunguka msitu wa Jambiani - Muyuni kwa ajili ya uhifadhi wa msitu huo.

"Ninawaomba wataalamu pindi mtakapomaliza mafunzo haya, muwe walimu kwa wananchi wa Jambiani-Muyuni na pia muwe tayari kushirikiana nao ili kwenda sambamba na matumizi hayo ya teknolojia katika kuondoa uhalifu unaotokea katika hifadhi hizo," alisema Miza.

Mratibu wa Taifa ya Programu ya Roots & Shoots iliyopo chini ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori ya Jane Goodall, Japhet Jonas Mwanang'ombe, alisema kuwapo maofisa misitu na maliasili na wataalamu wa taasisi nyingine kunatoa fursa ya kujadiliana kuhusiana na mpangokazi ambao utaanza kutekelezwa hivi karibuni.

Alisema kutokana na makubaliano kati ya Taasisi ya Jane Goodall na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu usimamizi wa misitu hususan katika msitu wa Jambiani - Muyuni, Taasisi ya Jane Goodall inatumia zaidi teknolojia katika kulinda misitu ambapo teknolojia hiyo itaenda kujua hali halisi ya uharibifu wa kimazingira wa misitu ya Zanzibar.

Alisema kuwa matumizi ya GIS yatawashirikisha wananchi wa vijiji vya Jambiani-Muyuni ambao watakuwa wadau kwenye usimamizi wa misitu sambamba na kuwapatia simu ambazo zitakuwa na mfumo utakaowasaidia kuona matukio yatakayotokea kupitia simu zao.

Mratibu huyo alisema wanatarajia kuwashirikisha wanafunzi wa shule mbalimbali za Unguja na Pemba kwa kuwapa elimu hiyo pamoja na kuwapatia semina walimu kuhusu uhifadhi wa misitu.

Katibu wa Jumuiya ya Uhifadhi na Maendeleo Kusini Unguja, Haji Ibrahim, alisema kuwapo kwa teknolojia hiyo kutasaidia kurahisisha kuwapata wahalifu ambao wanawarejesha nyuma katika juhudi zao za uhifadhi wa misitu.



Wanafunzi wanaosoma fani ya uchomeleaji wa vyuma katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Makunduchi wakimsikiliza Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA). Waziri Salum (hayupo pichani) alipowatembelea kuona maendeleo yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi awahakikishia ushirikiano wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imeeleza kuwa inathamini uamuzi wa wawekezaji kutumia mitaji yao kuendeleza sekta mbalimbali zinazochangia maendeleo ya nchi na watu wake.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza katika hafla ya chakula cha usiku baada ya ufunguzi wa Hoteli ya Emerald Hotel & Spa iliyoko Matemwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema kutokana na imani waliyoionyesha kwa Zanzibar, serikali itaendelea kuwapa ushirikiano ili wafanye uwekezaji mkubwa zaidi.

Dk. Mwinyi aliishauri Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kuzidisha juhudi za kuvutia uwekezaji zaidi katika kila sekta ili nchi ipige hatua zaidi za maendeleo.

"Ninapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza ZIPA kwa juhudi mnazozichukua na mnafanya kazi nzuri na endeleeni na kazi hii, hakikisheni mnavutia uwekezaji wa kila aina kwa sababu ili tupige hatua za kimaendeleo lazima tupate uwekezaji," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema faida nyingi zinapatikana ikiwamo ajira, soko la bidhaa zinazozalishwa nchini na huduma muhimu zinazotolewa na wawekezaji ikiwamo kujenga hospitali, shule na huduma za kijamii.

Hivyo, alisema ni vyema kushirikiana nao ili mafanikio hayo yapatikane ambayo yatasaidia kuimarisha maendeleo ya Zanzibar na watu wake.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alimwahidi Dk. Mwinyi wataendelea kumuunga mkono katika juhudi zake za kuinua sekta hiyo ili kufikia azma na malengo yaliyowekwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Shariff Ali Shariff, alisema jumla ya miradi 223 ya uwekezaji imesajiliwa na kuwekezwa nchini kwa kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya nane.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAZZAKI ABDULHAMID ESMAIL** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **LANDCRUISER PRADO** yenye usajili namba **T846 BNN,** CHASSIS NAMBA: **KDJ950036110** na ENGFINE NAMBA: **1KD0935146.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU.RB/40021/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na 82/ 2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU HABIBA SALUM ALLY**
**KATIKA SHAURI LA MAOMB YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA LATIFA MBARAKA MSHINDO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe15 Mwezi 2 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yoyote mwenyewe wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 19 mwezi 01 mwaka 2023**

## MNADA WA HADHARA/NOTISI

Tujijenge Tanzania Financial Services Ltd, tunatangaza notisi ya siku Thelathini (30) tangu tarehe ya tangazo hili gazetini kwa mdaiwa - Venance Costa Manji wa Dar Es Salaam aliyekopa na kushindwa kulipa deni la mkopo wake kulingana na makubaliano ya mkataba.

Unatakiwa kulipa deni lako lote ndani ya siku 30, na mara tu baada ya notisi hii kuisha bila kulipa mnada wa hadhara utaendeshwa na RAISSA COMPANY LIMITED kwa kuuza gari kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:-

| Mdaiwa/ mdhamini | Aina ya Dhamana | Tarehe ya mnada - Mahali |
|---|---|---|
| Venance Costa Manji | **T 101 DTN**, TOYOTA Crown Rangi Nyeusi | 03/03/2023 -Yard ya Raissa Co. Ltd KIMARA - DSM |

Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kukagua na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: 0652113262 / 0718068335**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**
**KATIKA SHAURI LA MADAI NA. 72/2022**
**ANTONI NYERERE.........MDAI**
**DHIDI**
**EDWIN KIFARU..........MDAIWA**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA EDWIN KIFARU**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Mahaka ya wilaya ya Morogoro tarehe 10/02/2023 saa 2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kusiklizwa.

Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI leo tarehe 23 Mwezi January 2023

E. C. LUKUMAI
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MOROGORO.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CONSTANCE THECLA SEMFUKO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 198 DNA – TOYOTA IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/41887/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIMBALIKAMBAKO COMPANY LIMITED** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 163 DPL** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi au apige simu **0683 284 671**. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/37014/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI

**STIGMATINE FATHERS** wanatangaza kupotea kwa Cheti cha Usajili Namba **So. 7386** kilichotolewa na Msajili wa Taasisi za Kijamii Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi au apige simu **0683 284 671**. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/36544/2023.**

## TANGAZO

**NYUMBA ZINAUZWA ARUSHA**

1) INA RUM 2 MASTA 1 MIL 40/= KIWANJA 20x20
2) INA RUM 2 MASTA 1 MIL 35/= KIWANJA 20X20
3) INA RUM 3 MASTA 1 MIL55/= KIWANJA 28X15
4) INA RUM 3 NYUMBA 2 ZIPODUKA BOVU MIL 100/= 39X70

**MAWASILIANO 0755907520/0787187794**


***OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710.***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# IHC sasa kuwekeza dola bilioni 400 FPO

**Na Maulid Mmbaga**

KAMPUNI ya uwekezaji ya kimataifa (IHC) imetangaza kuwekeza dola bilioni 400 kwa kampuni ya kibiashara ya (FPO) ya nchini India, huku ikiahidi kuwa itaendelea kuchunguza fursa za biashara maeneo tofauti kama Ulaya, Afrika, Asia na Amerika Kusini ndani ya mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na IHC, uwekezaji wake wa kwanza mwaka huu unakuja wakati kampuni ikiendelea kuongeza na kubadilisha uwekezaji wake ndani na nje ya nchi, ikilenga katika masoko ya bara la Ulaya, Afrika, Asia na Amerika Kusini.

Ofisa Mkuu Mtendaji wa IHC, Syed Basar Shueb, alisema imani yao wanaona uwezekano mkubwa wa ukuaji kutoka kwa mtazamo wa muda mrefu na kuongeza thamani kwa wanahisa wao.

Alisema huo ni mkataba wao wa pili wa uwekezaji na Kampuni ya Adani Group ya India baada ya uwekezaji wa 2022 wa dola bilioni mbili katika makampuni matatu, ambayo ni Adani Green Energy, Adani Transmission na Adani Enterprises, ambazo zote zimeorodheshwa kwenye soko la hisa la Bombay na la kitaifa la India.

"Faida ya FPO ni marejeleo ya kihistoria ya ripoti ya mapato ya kampuni, usimamizi wa kampuni, mbinu za biashara na data nyingi za kuhifadhi kabla ya kufanya uamuzi wowote wa uwekezaji," alisema Shueb.

Aidha, alieleza kuwa IHC inaendelea kutazamia mwaka huu wakati mkakati wake wa maendeleo unapoendelea, huku kukiwa na upataji zaidi unaotarajiwa katika mabara manne ifikapo mwisho wa mwaka huu, ukilenga uchumi unaokua kwa kasi, masoko ya hisa yanayopanuka kwa kasi na kivutio kikuu cha uwekezaji.

"Tunatazama soko la kimataifa kwa karibu kwa matarajio mapya na tutaendelea kutafuta fursa zaidi nje ya soko letu la ndani ya 2023," alisema Shueb.

Alisema IHC inalenga kuongeza upatikanaji wake wa kimataifa kwa asilimia 70 katika mwaka huu na sekta ya nishati safi na usindikaji wa chakula kuwa lengo kuu.

**Tunatazama soko la kimataifa kwa karibu kwa matarajio mapya na tutaendelea kutafuta fursa zaidi nje ya soko letu la ndani ya 2023**

# Zelensky, 2023 utakuwa wa ushindi kwa Ukraine

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amesema ana uhakika nchi yake inaweza kuishinda Urusi mwaka huu, licha ya changamoto wanayokumbana nayo katika uwanja wa mapambano.

Akilituhubia taifa hilo usiku wa kuamkia jana, Zelensky alikiri kuwa hali bado ni ngumu, kutokana na mapigano makali mashariki mwa nchi hiyo.

"Hali katika eneo la mapambano ni mbaya, hasa kwenye jimbo la Donetsk na maeneo ya kusini. Miji ya Bakhmut, Vuhledar na maeneo mengine katika jimbo la mashariki la Donetsk, inaendelea kushambuliwa kwa makombora ya kila mara ya Russia," alisema Zelensky.

Pia alisema Ukraine inahitaji haraka silaha mpya ili kukabiliana na mashambulizi ya mara kwa mara ya majeshi ya Russia huko Donetsk, huku akiwasisitiza washirika wake kuongeza kasi ya upelekaji wa silaha, kutokana na kwamba hali nchini mwake bado ni mbaya.

**Watu wanne pia wameuawa katika mkoa wa Zaporizhzhia, ambako mapambano yalipamba moto katika siku za hivi karibuni.**

Zelensky alisema Russia inataka vita viendelee na inajaribu kuvidhoofisha vikosi vya Ukraine.

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, alisema nchi yake haitopeleka ndege za kivita katika taifa hilo, huku katika mahojiano yake na gazeti la Tagesspiegel, Scholz akionya kuhusu hatari ya kuongeza mvutano, wakati Russia ikiwa tayari imelaani vikali ahadi ya kupelekwa vifaru hivyo.

Naye Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Ryabkov, alisema kuwa baada ya Marekani kuamua kuipatia vifaru Ukraine, hakuna haja ya Russia kuzungumza na Ukraine au washirika wake wa Magharibi.

Ryabkov alisema hakuna mtu katika nchi za Magharibi ambaye amekuja na mipango yoyote madhubuti ya kuutatua mzozo wa Ukraine.

Aidha, Rais Zelensky, alisema watu watatu waliuawa katika mji wa Kherson, mmoja wa Kharkiv, juzi na sita kujeruhiwa katika shambulizi la kombora la Russia.

"Watu wanne pia wameuawa katika mkoa wa Zaporizhzhia, ambako mapambano yalipamba moto katika siku za hivi karibuni," alisema.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kujihami ya NATO, Jens Stoltenberg, alitoa wito kwa Korea Kusini kuongeza msaada wake wa kijeshi kwa Ukraine. **DW**




Eneo la uchifu wa Walese Vonkutu, linalotajwa kuvamiwa huku maduka yaliyoko kando mwa barabara yakionekana kufungwa. **PICHA: AFP**

# 15 wauawa mashambulizi mapya DRC

**KINSHASA,** DRC

WANAKIJIJI takribani 15 wameuawa katika kijiji cha Ituri nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) katika uvamizi uliofanyika kwenye mpaka wa Uganda.

Inaelezwa kuwa mashambulizi hayo mapya yaliyotekelezwa mwishoni mwa juma lililopita yanahusishwa na kundi la Allied Democratic Forces (ADF), moja ya makundi yenye silaha ambayo yamefanya uharibifu mkubwa na kumwaga damu katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa mashirika ya kiraia, miongoni mwa waathiriwa ni dazeni ya wanawake na mtoto wa takriban miaka miwili, na kwamba watu wenye silaha walilenga vijiji vitatu kwa wakati mmoja muda mfupi kabla ya kupambazuka kabla ya kuzuiwa na jeshi.

Pia ilitajwa kuwa maeneo haya ni sehemu ya uchifu wa Walese Vonkutu, eneo ambalo lilishuhudia umwagaji damu wiki mbili zilizopita. **RFI**

# 28 wauawa mlipuko msikitini

**PESHAWAR,** Pakistan

TAKRIBANI watu 28 wameuawa katika mlipuko uliotokea kwenye msikiti mmoja katika mji wa Peshawar nchini Pakistan na kwamba ulitokea wakati msikiti huo ukiwa umejaa waumini na zaidi ya watu 150 wamejeruhiwa.

Mlipuko huo ulitokea wakati wa sala ya alasiri katika mji wa kaskazini magharibi, karibu na mpaka wa nchi hiyo na Afghanistan.

Inaelezwa kuwa sehemu ya jengo la msikiti huo iliharibiwa na maofisa wa usalama walisema watu wamezikwa chini ya vifusi, na kwamba wengine kadhaa walipelekwa katika hospitali za mji huo.

Waziri Mkuu wa Pakistan, Shebaz Sharif, alilaani vikali shambulio hilo, licha ya kudaiwa kwamba chanzo cha mlipuko huo hakijajulikana.

Kwa mujibu wa taarifa ya Sharif, waliohusika na tukio hilo hawana uhusiano wowote na Uislamu na kwamba taifa hilo zima limesimama kwa umoja dhidi ya tishio la ugaidi.

Msemaji wa Hospitali ya Lady Reading Mohammad Asim, alisema kuwa baadhi ya waliojeruhiwa walikuwa katika hali mbaya ya dharura.

Vyombo vya habari vya ndani vinaripoti kuwa polisi, jeshi na vikosi vya kutegua mabomu viko kwenye eneo la tukio.

Katika mji mkuu, Islamabad Polisi ilitoa tahadhari ya juu ya usalama na kusema usalama katika maeneo yote ya kuingia na kutoka katika mji huo umeongezeka. **BBC**

HABARI MICHEZO

# MUSONDA AWAAHIDI YANGA MABAO ZAIDI

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kufunga mabao mawili kwenye mechi ya 32 bora ya Kombe la FA dhidi ya Rhino Rangers juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, straika wa Yanga, Kennedy Musonda, amewaahidi wanachama na mashabiki wa timu hiyo mabao zaidi kwenye michuano mbalimbali ambayo itacheza.

Musonda raia wa Zambia alisema hayo baada ya kufunga mabao hayo mawili ikiwa ni mara ya kwanza kufanya hivyo tangu ajiunge na klabu hiyo siku kadhaa zilizopita kwenye kipindi cha dirisha dogo.

Mabao yangu yote mazuri, lakini nimelipenda la kwanza na ukiwa kwenye timu kubwa kama hii ni lazima kichwa kitulie, kwa sababu ina wanachama na mashabiki wengi ambao wanategemea kitu kutoka kwako. Namshukuru Mungu nilikuwa na presha ya kufunga mabao, nina furaha nimefunga mabao haya ambayo yamenipa kujiamini na sasa naamini mabao mengi yatakuja.

**Nawaahidi Wanayanga mabao zaidi, ushindi na mchezo bora," alisema Musonda.**

Alisema pamoja na kuwa na hamu ya kufunga, lakini hakuwa na wasiwasi sana na lilikuwa ni suala la muda tu yeye kufanya hivyo.

"Unajua mshambuliaji unapokuwa uwanjani unatarajia muda wowote utafunga, lakini kama hukupata bao unatakiwa uamini tu kuwa mechi ijayo utafunga," alisisitiza.

Ilimchukua dakika 16 kupachika bao lake la kwanza kwenye mechi hiyo, likiwa la pili kwenye mchezo, lingine akifunga dakika ya 46.

Mabao mengine kwenye mechi hiyo ambayo Yanga ilishinda mabao 7-0, yalifungwa na Dickson Ambundo, Stephane Aziz Ki, Farid Mussa, Yannick Bangala, na David Brayson.

Musonda ambaye alisajiliwa na Yanga kipindi cha dirisha dogo la usajili akitokea klabu ya Power Dynamos ya Zambia, hakufunga kwenye mechi mbili za mwanzo za Ligi Kuu ambazo timu yake ilicheza, akiingia kipindi cha pili kwenye mechi dhidi ya Ihefu Januari 26 ambapo ilishinda bao 1-0, na alianza kwenye mechi ambayo Yanga ilicheza dhidi ya Ruvu Shooting na kushinda bao 1-0, mechi zote zikicheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kutofunga bao lolote kwenye mechi hizo mbili kulianza kuleta minong'ono kwa baadhi ya mashabiki wa soka.



Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Taifa, Ramadhan Matola, akishiriki ujenzi wa ukuta wa uwanja wa mpira wa miguu wa Kassim Majaliwa, mjini Ruangwa juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 46 ya kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), yanayofikia kilele chake Februari 5, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Singida yapania kuishusha Simba

Na Hadija Mngwai

TIMU ya Singida Big Stars ipo jijini Dar es Salaam ikiendelea kujiwinda na mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba ambapo wametamba kuhakikisha wanafanikiwa kuibuka na ushindi katika mchezo wao Februari 3.

Singida ambayo ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara inatarajia kushuka dimbani Ijumaa katika Uwanja wa Benjamini Mkapa ambapo wamejipanga kuhakikisha wanafanikiwa kuibuka na pointi tatu.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, amesema kuwa wanajiandaa kushinda mchezo huo licha ya kuwakosa nyota wao wawili Deus Kaseke na Mbrazil, Dario Frederio katika mchezo huo.

"Tunajiandaa vyema na mchezo wetu dhidi ya Simba tutakaocheza Februari 3, timu inafanya mazoezi katika Uwanja wa Polisi Temeke, morali ya wachezaji kuelekea mchezo huo ipo juu kila mmoja anahitaji kupata matokeo mazuri.

"Kocha Hans anaendelea kukisuka kikosi chake kuhakikisha wachezaji wanakuwa na kiwango kizuri kutofautisha na walichokionyesha katika mchezo uliopita dhidi ya Ruvu Shooting ambapo kocha hakufurahishwa nacho licha ya kupata matokeo mazuri," alisema Massanza.

Aidha, aliongeza kuwa, katika mchezo huo wanatarajia kumkosa Kaseke ambaye anatumikia adhabu yake ya kufungiwa michezo mitatu ambapo tayari ameshakosa dhidi ya Ruvu Shooting kisha mchezo unaofuata dhidi ya Simba na Ihefu huku Dario akiwa Brazil kwa ruhusa maalumu.

# Gwambina yaondolewa, yashushwa daraja, yafungiwa

Na Adam Fungamwango

KAMATI ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), imeiondoka klabu ya Gwambina kwenye Ligi ya Championship, na kupewa adhabu ya kushushwa daraja na kufungiwa kucheza ligi kwa misimu miwili, baada ya kuthibitisha yenyewe kujitoa.

Kwenye kikao chake ilichokaa Januari 26 mwaka huu, kamati hiyo ilikaa kujadili shauri la klabu hiyo kutaka kujitoa, baada ya kushindwa kucheza mechi nne mfululizo za ligi hiyo.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi imesema kuwa mbali na hayo, michezo yote ambayo timu hiyo imecheza imefutwa kwa sababu idadi ya mechi kwa timu husika haikufika zaidi ya nusu ya michezo yake kwenye msimu huu wa Ligi ya Championship.

Michezo ambayo haikushiriki kwa mujibu wa ratiba ya ligi hiyo ni dhidi ya African Sports, Mbuni FC, Fountain Gate, JKT Tanzania na Mbeya Kwanza.

Taarifa imesema, awali mmiliki wa klabu hiyo, Alexander Mnyeti, alitangaza uamuzi wa kutoendelea na ligi hiyo kupitia vyombo vya habari na baada ya taarifa hiyo, Bodi ya Ligi iliitaka klabu ya Gwambina kuthibitisha kwa maandishi kauli ya mmiliki wake hadi kufika Januari 20 mwaka huu, lakini haikufanya hivyo.

Baada ya hapo, taarifa hiyo imesema kuwa, Sekretarieti ya Bodi ya Ligi ililipeleka shauri hilo kwenye Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ambayo baada ya kupitia vielelezo na shauri husika, ilithibitisha klabu ya Gwambina kujitoa kwenye Ligi ya Championship.

Timu hiyo iliyoanzishwa mwaka 2019 yenye maskani yake Misungwi, ikiwa ni moja kati ya timu chache nchini zilizokuwa zikimiliki uwanja wake wa kucheza mechi.

Ilipanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, lakini ilishuka msimu huo huo ambapo msimu huu ilikuwa ikipambana kutaka kurejea tena Ligi Kuu.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA NA ENZO

CHELSEA wamefufua tena mazungumzo na Benfica ili kujaribu kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 22, kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa leo. ***(Telegraph)***

### SPURS YAMTAKA HINCAPIE

KLABU ya Tottenham Hotspur imewasilisha ofa ya maneno ya euro milioni 25 kwa Bayer Leverkusen kwa ajili ya uhamisho wa beki wa kati wa Ecuador, Piero Hincapie mwenye umri wa miaka 21. ***(Bild)***

### SHELVEY AWANIWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest iko mbioni kumsajili kiungo wa kati wa Newcastle United, Jonjo Shelvey mwenye umri wa miaka 30. ***(Telegraph)***

### FELIX ATAKIWA BARCA

BARCELONA inamfuatilia mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 23, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Chelsea. ***(Sport)***

### LINDELOF AWINDWA INTER

INTER Milan inamtaka mlinzi wa Manchester United na Sweden, Victor Lindelof mwenye umri wa miaka 28 kama mbadala wa Milan Skriniar ikiwa beki huyo wa Slovakia mwenye umri wa miaka 27 atahamia Paris St-Germain. ***(Fabrizio Romano)***

### JUDE MDOGO AWANIWA

KLABU ya Tottenham Hotspur inashughulikia mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa Birmingham City, Jobe Bellingham mwenye umri wa miaka 17, ambaye ni mdogo wa kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19. ***(Football Insider)***

### AKARIBIA GALATASARAY

KLABU ya Galatasaray inaongoza katika mbio za kutaka kumsajili beki wa Liverpool, Nat Phillips mwenye umri wa miaka 25 ambaye thamani yake ni pauni milioni 10. ***(Athletic)***

### BECAO ANYATIWA

KLABU ya Everton inapania kumsajili nyota wa Udinese na Brazil mwenye umri wa miaka 27, Rodrigo Becao. ***(Mail)***

### NAVAS ATAKIWA

KLABU ya Nottingham Forest ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili kipa wa Paris St-Germain na Costa Rica, Keylor Navas mwenye umri wa miaka 36. ***(Football Insider)***

### BELLERIN KUBADILISHWA

SPORTING Lisbon inakaribia kufikia kumsajili kwa mkopo beki wa Barcelona na Hispania, Hector Bellerin, 27, kama mbadala wa Pedro Porro, 23, ambaye Tottenham wanatarajia kumsajili. ***(Atheletic)***

### MARTINEZ AGOMBEWA

MANCHESTER City itapambana na Barcelona katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa Girona na Hispania umri wa chini ya miaka 21, Arnau Martinez mwenye umri wa miaka 19. ***(Mundo Deportivo)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA YAKOMAA NA ENZO FERNANDEZ

**LONDON,** England

CHELSEA imewaambia Benfica kuwa watalipa kiasi cha pauni milioni 106 kwa ajili ya kumsajili Enzo Fernandez kwa awamu huku wakipania kupata huduma yake kabla ya dirisha la Januari kufungwa leo, kwa mujibu wa Daily Mail.

**Chelsea, ambao walithibitisha kumsajili Malo Gusto kwa pauni milioni 26.3 kutoka Lyon Jumapili, walikuwa na ofa ya takriban pauni milioni 75 pamoja na bonasi kwa Fernandez ambayo ilikataliwa mapema mwezi huu.**

Wababe hao wa Ligi Kuu England jana Jumatatu walitarajia kusafiri hadi Ureno kuandaa duru mpya ya mazungumzo na Benfica na kutoa ofa ya kulipa pauni milioni 106 kwa awamu kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

Kwa mujibu wa Futebol, Chelsea

**● ● ● Yatuma ujumbe mzito nchini Ureno kwa ajili ya kumalizana na Benfica huku...**

imetuma wawakilishi jijini Libson ili kufunga mkataba na Benfica kabla ya dirisha la usajili la Januari kufungwa.

Chelsea inaripotiwa kutoa kulipa kwa mjumbe huyo mwenye umri wa miaka 22 kwa pauni milioni 106 kwa awamu kwa kuwa wako chini ya shinikizo la kukamilisha dili ndani ya saa 48 zijazo.

Uamuzi huo umekuja baada ya Benfica kukataa ofa ya awali ya Chelsea ya takriban pauni milioni 75 pamoja na bonasi mapema mwezi huu. Benfica ilitaka kipengele kamili cha kuachiliwa kilipwe hapo awali, badala ya pendekezo la Chelsea ambapo wangelipa pauni milioni 37.3 kwa miaka mitatu.

Hata hivyo, Chelsea wanatumaini wataweza kukubaliana na timu hiyo ya Ureno watakapokutana mjini Lisbon. Benfica ilitoa taarifa mwishoni mwa Desemba ikisisitiza kwamba Fernandez atasalia nao hadi mwisho wa msimu wa 2022-23.

"SL Benfica inafafanua kwamba hakuna wakati Rais wa Klabu, Rui Costa, alitamka maneno ambayo yanasambazwa nchini Italia na DAZN," klabu hiyo ilisema.

"Sport Lisboa e Benfica inasisitiza nia yake ya kumtegemea mchezaji Enzo Fernández hadi mwisho wa msimu."

Chelsea tayari wameimarisha kikosi chao mwezi huu kwa kusajili wachezaji kadhaa - wakiwamo David Datro Fofana, Benoit Badiashile, Andrey Santos, Joao Felix, Mykhailo Mudryk, Noni Madueke na Malo Gusto.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,072,5

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 01,02 NA 03 FEBRUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/02/23 | 22:00 | Waalwick vs GO Ahead Eagles | 2.30 | 3.37 | 2.87 |
| 02. 01/02/23 | 22:15 | Grasshoppers vs FC Basel | 2.79 | 3.31 | 2.27 |
| 03. 01/02/23 | 22:45 | Oxford Utd vs Barnsley | 2.49 | 3.34 | 2.64 |
| 04. 01/02/23 | 22:45 | Kilmarnock vs Dundee Utd | 2.21 | 3.29 | 3.14 |
| 05. 02/02/23 | 02:00 | Tlaxcala FC vs Alebrijes De Oaxaca | 2.52 | 3.01 | 2.70 |
| 06. 02/02/23 | 06:05 | Club Atletico La Paz vs Cimarrones De Sonora | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 07. 02/02/23 | 17:00 | Kayserispor vs Basaksehir | 2.70 | 3.39 | 2.44 |
| 08. 02/02/23 | 17:00 | Chennaiyin FC vs Delhi Dynamos FC | 2.40 | 3.42 | 2.56 |
| 09. 02/02/23 | 20:00 | Adana Demirspor vs Fenerbahce | 2.92 | 3.51 | 2.23 |
| 10. 02/02/23 | 20:00 | Anorthosis Famagusta vs Omonia Nicosia | 2.76 | 3.24 | 2.51 |
| 11. 02/02/23 | 22:45 | Zulte Waregem vs Mechelen | 2.63 | 3.42 | 2.42 |
| 12. 03/02/23 | 06:00 | San Luis vs Puebla FC | 2.32 | 3.19 | 3.03 |
| 13. 03/02/23 | 14:00 | Tiddim Road Athletic Club vs Mohammedan SC | 2.39 | 3.28 | 2.65 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LICHA YA SARE ANCELOTTI APONGEZA KIWANGO



**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti alisifu uchezaji "kamili" wa Real Madrid, licha ya sare ya bila kufungana kwenye Ligi Kuu ya Hispania, ya La Liga, dhidi ya Real Sociedad, Jumapili.

Madrid wapo nyuma kwa pointi tano nyuma ya vinara Barcelona baada ya kushindwa kuvuka safu ya ulinzi ya kikosi hicho cha Kocha Imanol Alguacil katika mechi ya upande mmoja iliyochezwa kwenye dimba la Santiago Bernabeu.


Kipa wa Sociedad, Alex Remiro, aliokoa hatari saba langoni mwake, idadi kubwa zaidi ambayo kwenye mchezo mmoja wa La Liga msimu huu, ikiwa ni pamoja na mipira mitatu ya adhabu ndogo ya Vinicius Junior.

Alisema: "Ilikuwa aibu kwa sababu tulicheza vizuri sana na tulistahili kushinda. Tulicheza mchezo kamili, moja ya mechi bora zaidi ya msimu, lakini hatukuwa na bahati yoyote.

"Timu inaimarika na inakua na kimwili tuko vizuri zaidi. Sasa majeruhi wanarejea na tuna imani kwa miezi ijayo.

"Tumefanya vizuri sana na bila mpira na tulichotakiwa kufanya ni kufunga, tulikaribia sana, lakini ni sare. Nimeridhika kwa sababu timu imecheza vizuri sana."

Sehemu kubwa ya tishio la kushambulia la Madrid lilitokana kwa Vinicius, ambaye alijaribu kupiga chenga 21 nyingi zaidi kwa mchezaji mmoja katika mechi moja ya La-Liga tangu msimu wa 2005-06.




## *Mourinho aipa Napoli ubingwa*

**ROME,** Italia

JOSE Mourinho alidai kuwa Roma walipata kichapo "kisicho cha haki" kutoka kwa vinara wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Napoli huku akiwatabiria kushinda taji hilo msimu huu.

Mourinho hakuweza kuwa bora mbele ya kikosi cha kocha, Luciano Spalletti ambapo sasa Napoli wapo kileleni mwa msimamo wa ligi kwa tofauti ya pointi 13 baada ya michezo 20.

Roma walio nafasi ya sita wangekuwa pointi sawa na Inter, ambao wanashika nafasi ya pili kama wangepata ushindi uliopigwa Uwanja wa Diego Armando Maradona.

Victor Osimhen alifunga krosi ya Khvicha Kvaratskhelia na kuifanya Napoli kuongoza katika dakika ya 17, lakini Roma walisawazisha dakika ya 75 kupitia kwa Stephan El Shaarawy.

Hata hivyo, Roma hawakuweza kushikilia pointi moja, Giovanni Simeone akaipa bao la ushindi dakika ya 86 alipopokea pasi fupi kutoka kwa Piotr Zielinski.

Mourinho alisema: "Tangu dakika ya kwanza tulicheza vizuri. Timu ilikuwa ikitawala kila wakati.

"Napoli waliteseka, sisi ndio timu iliyowatia hofu zaidi. Wakati mwingine mpira wa miguu sio wa haki, timu ambayo inastahili kushinda inapoteza.

## HABARI MICHEZO

49,524/-

# TAASISI YA MPIRA WA KIKAPU AFRIKA KUJENGA VIWANJA

**Na Faustine Feliciane**

KATIKA kuadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwa Taasisi ya 'Giant of Africa', taasisi hiyo imedhamiria kuendelea kuboresha na kujenga viwanja vya mchezo wa mpira wa kikapu katika nchi za Afrika ili kuwapa fursa vijana kucheza mchezo huo.

Mwanzilishi mwenza wa Giant of Africa ambaye ni makamu wa Rais wa klabu ya mpira wa kikapu ya Marekani ya Toronto Raptors, Masai Ujiri, alisema maadhimisho ya miaka hiyo 20 yatafanyika katika maeneo mbalimbali na kwa Afrika wataadhimisha kwa kuendesha kambi za mpira wa kikapu kwa wavulana na wasichana, kujenga viwanja vya mchezo na kuwezesha mipango ya kuwafikia vijana wengi.

"Imekuwa jambo la unyenyekevu kufikia hatua hiyo ya ajabu na kuna mengi ya kujivunia tunapotafakari kuhusu miongo miwili iliyopita, miaka 20 ya utumishi imewezekana tu kwa sababu ya shauku na kujitolea kwa kila mtu na jamii ambayo imekusanyika kufanya Giants of Africa kama ilivyo leo," alisema Ujiri na kuongezea.

"Kwa kweli ndio tumeanza..., kuna ufahamu ambao tunahitaji kuendelea na hamu ya kujifunza kutoka kwa safari yetu ili tuweze kuendelea kusaidia zaidi, tunafurahia mustakabali mzuri huku Giants of Africa ikiendelea kukuza miundombinu na kuwatia moyo vijana wa Kiafrika duniani kote kwa programu zinazolenga elimu, uwezeshaji na uongozi, ndani na nje ya viwanja, " alisema Ujiri.


Taasisi hiyo hapa nchini imefanikisha kujenga kiwanja cha mpira wa kikapu katika Shule ya Sekondari ya Minaki iliyopo Kisarawe.

Uwanja huo ulizinduliwa na Rais mstaafu Jakaya Kikwete kwa mwaliko wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo.

Katika mwendeleze wa maadhimisho ya miaka hiyo 20, Giant of Africa imeandaa tamasha kubwa litakalohusisha vijana zaidi ya 250 kutoka nchi 16 za Afrika ambapo mafunzo mbalimbali ya mpira wa kikapu yatatolewa pamoja na burudani mbalimbali.

Tamasha hilo litafanyika Kigali, Rwanda Agosto 13-19 katika ukumbi mkubwa wa michezo wa BK Arena.

Tangu mwaka 2003, Giant of Africa imewafikia vijana zaidi ya 40,000 katika nchi mbalimbali za Afrika kupitia programu ya ujenzi wa viwanja 30 na vituo 80 vya mpira wa kikapu.



Mchezaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki (kulia), akipiga hesabu za kumtoka mlinzi wa Rhino Rangers wakati wa mchezo wa Kombe la FA hatua ya 32 bora baina ya timu hizo uliopigwa juzi Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: YANGA**

## Rais wa Yanga atoa neno kuhusu Fei Toto

INATOKA UKURASA 24

umiliki wa mchezaji.

"Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji iliweza kutoa maamuzi hayo kwa hiyo sisi kama wazazi tunaendelea kumwacha na hali yake na hakuna kitu chochote nachoweza kusema kipo katika wakati mbaya.

## *Mangungu: Sasa kazi ni moja*

INATOKA UKURASA 24

nyesha namba ambavyo wanachama wana imani na utendaji wake.

Aidha, amewapongeza wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi waliochaguliwa kwenye uchaguzi iliofanyika Jumapili jijini Dar es Salaam.

Rais huyo alisema TFF itaendelea kushirikiana na klabu hiyo katika maendeleo ya mpira wa miguu na anaamini chini ya uongozi wao, klabu hiyo itaendelea kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika ambako kwa sasa wapo kwenye hatua ya makundi, ili kuendelea kuipeperusha vema bendera ya Tanzania nje ya mipaka ya Tanzania.

Mangungu alichaguliwa na wanachama wa klabu hiyo kuiongoza tena klabu hiyo kubwa na kongwe kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, lakini viongozi wa Bodi ya Wakurugenzi waliochaguliwa ni Sk. Seif Ramadhani Muba, Asha Baraka, CPA Issa Masoud, Dk. Rodney Chiduo na Selemani Haroub.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/02/23 | 18:00 | Preston North End vs Bristol City | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 02. 04/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Queens Park Rangers | 3.00 | 3.20 | 2.39 |
| 03. 04/02/23 | 18:00 | Reading FC vs Watford FC | 2.70 | 3.20 | 2.60 |
| 04. 04/02/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KVC Westerlo | 2.75 | 3.45 | 2.41 |
| 05. 04/02/23 | 22:00 | FC Emmen vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 04/02/23 | 23:00 | Excelsior Rotterdam vs RKC Waalwijk | 2.70 | 3.35 | 2.49 |
| 07. 04/02/23 | 23:00 | Stade Rennes vs Lille OSC | 2.30 | 3.35 | 2.95 |
| 08. 04/02/23 | 23:30 | Estoril Praia vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 09. 05/02/23 | 03:30 | Atletico Lanus vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.31 | 2.85 | 2.80 |
| 10. 05/02/23 | 03:30 | Argentinos Juniors vs Racing Club Avellaneda | 2.60 | 2.70 | 2.60 |
| 11. 05/02/23 | 15:30 | Royal Antwerp FC vs Club Brugge | 2.49 | 3.40 | 2.65 |
| 12. 05/02/23 | 16:00 | Villarreal CF B vs Granada CF | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 13. 05/02/23 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.49 | 3.15 | 2.37 |
| 14. 05/02/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs NEC Nijmegen | 2.40 | 3.35 | 2.85 |
| 15. 05/02/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Leeds United | 2.60 | 3.30 | 2.60 |
| 16. 05/02/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs FC Nantes | 2.65 | 3.10 | 2.70 |
| 17. 05/02/23 | 17:00 | Torino FC vs Udinese Calcio | 2.24 | 3.20 | 3.25 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 31/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 1663 | Alanyaspor vs Sivasspor | 2.02 | 3.50 | 3.39 |
| 19:00 | 4857 | Algeria vs Niger | 1.49 | 3.85 | 7.20 |
| 20:00 | 2559 | Paderborn vs Stuttgart | 2.84 | 3.49 | 2.37 |
| 20:00 | 4051 | Fatih Karagumruk vs Besiktas | 3.67 | 3.61 | 1.90 |
| 21:00 | 5663 | FC Thun vs FC Luzern | 3.42 | 3.42 | 1.94 |
| 21:00 | 5784 | Viseu vs Benfica Lisbon B | 1.72 | 3.68 | 4.31 |
| 22:00 | 2265 | Senegal vs Madagascar | 1.77 | 3.19 | 5.18 |
| 22:00 | 2424 | Pacos Ferreira vs Gil Vicente | 2.84 | 3.14 | 2.47 |
| 22:45 | 1128 | Solihull Moors vs Notts County | 4.95 | 4.21 | 1.55 |
| 22:45 | 1369 | Metz vs Rodez Aveyron | 1.64 | 3.51 | 5.35 |
| 22:45 | 1500 | Cove Rangers vs Ayr United | 3.11 | 3.32 | 2.10 |
| 22:45 | 2147 | Laval vs Dijon | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 22:45 | 2188 | Aldershot vs Boreham Wood | 2.69 | 3.22 | 2.49 |
| 22:45 | 2527 | Bastia vs St Etienne | 2.53 | 3.02 | 2.83 |
| 22:45 | 2804 | Inverness vs Queens Park | 2.50 | 3.32 | 2.51 |
| 22:45 | 3181 | Annecy FC vs Caen | 3.11 | 3.01 | 2.34 |
| 22:45 | 3204 | Grenoble Foot vs US Quevilly Rouen | 2.34 | 2.92 | 3.22 |
| 22:45 | 3280 | Kidderminster vs Blyth Spartans | 1.52 | 3.78 | 5.59 |
| 22:45 | 3409 | The New Saints vs Bala Town | 1.23 | 5.59 | 9.11 |
| 22:45 | 3493 | Luton Town vs Cardiff | 1.93 | 3.27 | 3.91 |
| 22:45 | 3632 | Leiston vs Ilkeston Town FC | 1.40 | 4.56 | 6.01 |
| 22:45 | 3724 | Dover vs Worthing | 2.74 | 3.21 | 2.36 |
| 22:45 | 3811 | Harrow Borough vs Halifax | 4.46 | 3.89 | 1.62 |
| 22:45 | 3821 | Warrenpoint vs Knockbreda | 1.25 | 5.40 | 8.93 |
| 22:45 | 3935 | Woking vs Torquay | 1.42 | 4.41 | 6.51 |
| 22:45 | 3972 | Needham Market vs Alvechurch | 1.94 | 3.42 | 3.42 |
| 22:45 | 3993 | Tamworth vs St Ives Town | 1.40 | 4.65 | 5.78 |
| 22:45 | 4094 | Eastleigh vs Barnet | 2.27 | 3.42 | 2.84 |
| 22:45 | 4112 | Niort vs Amiens | 3.07 | 3.02 | 2.36 |
| 22:45 | 4202 | Liversedge vs Gainsborough | 5.59 | 4.14 | 1.47 |
| 22:45 | 4288 | Loughgall vs Ballyclare | 1.41 | 4.35 | 6.22 |
| 22:45 | 4356 | Bordeaux vs Le Havre | 2.31 | 3.02 | 3.17 |
| 22:45 | 4475 | Salford City vs Walsall | 2.26 | 3.12 | 3.17 |
| 22:45 | 4691 | Sochaux vs Valenciennes | 1.81 | 3.36 | 4.35 |
| 22:45 | 4765 | Carlisle vs Barrow | 2.11 | 3.22 | 3.37 |
| 22:45 | 4831 | Paris FC vs PAU FC | 1.97 | 3.22 | 3.81 |
| 22:45 | 4838 | Union Berlin vs VfL Wolfsburg | 2.33 | 3.22 | 3.12 |
| 22:45 | 4883 | Crewe vs Stockport | 5.15 | 3.71 | 1.62 |
| 22:45 | 5174 | Lewes vs Wingate and Finchley | 1.58 | 3.97 | 4.65 |
| 22:45 | 5233 | Herne Bay vs Potters Bar Town | 2.80 | 3.63 | 2.14 |
| 22:45 | 5250 | Yeovil vs Wealdstone | 2.51 | 3.11 | 2.74 |
| 22:45 | 5257 | Ross County vs Hibernian | 3.54 | 3.44 | 1.99 |
| 22:45 | 5402 | South Shields vs Marske United FC | 1.23 | 5.18 | 10.37 |
| 22:45 | 5431 | Guingamp vs Nimes | 2.09 | 3.21 | 3.46 |
| 22:45 | 5644 | Royston Town vs Nuneaton | 3.06 | 3.63 | 2.01 |
| 22:45 | 5923 | Spennymoor Town vs Hereford United | 2.22 | 3.27 | 2.91 |
| 23:00 | 3787 | Inter vs Atalanta | 1.90 | 3.50 | 3.82 |
| 23:00 | 4209 | AC Siena vs Pontedera | 2.08 | 2.98 | 3.94 |
| 23:00 | 5294 | Newcastle vs Southampton | 1.42 | 4.28 | 7.17 |
| 23:00 | 5660 | Paraguay U20 vs Venezuela U20 | 1.94 | 3.21 | 3.68 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipas

Jumanne Januari 31, 2023






Chelsea yakomaa na Fernandez UKURASA 21





Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu akizungumza. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mangungu: Sasa kazi ni moja tu Simba SC

**Aahidi kufanikisha malengo ya Simba kimataifa, aomba mawazo ya mpinzani wake, TFF yawapongeza...**

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukamilika kwa uchaguzi wa Klabu ya Simba na Mwenyekiti, Murtaza Mangungu kutetea nafasi yake kwa kipindi kingine cha miaka minne, amesema sasa kinachofuata ni kazi moja ya kufanikisha malengo ya timu hiyo.

**Mangungu amechanguliwa kwa mara nyingine baada ya kufanikiwa kumshinda Adv. Mosses Kaluwa kwa kura 1,311 dhidi ya 1,045 alizopata mpinzani wake katika uchaguzi mkuu uliofanyika juzi, kwenye ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.**

Baada ya Kamati ya Uchaguzi wa Simba, iliyoongozwa na Mwenyekiti wake, Boniface Lihamwike, kukamilisha kuhesabu kura zilizopigwa walitangaza matokeo hayo alfajiri ya jana saa 11:00 kuwa Mangungu ametetea nafasi yake.

Matokeo ya uchaguzi huo yalichelewa kutangazwa kutokana na zoezi la kuhesabu kura kuchukuwa muda mrefu kutokana na idadi kubwa ya wanachama waliojitokeza ambao ni 2,363 kupiga kura huku halali zikiwa, 2,356 huku saba zikiharibika.

Akizungumza baada ya kutangazwa kushinda nafasi hiyo, Mangungu alisema kwa sasa anawataka na kuwahimiza wanasimba wote kuwa kitu kimoja na kushirikiana katika kufanikisha malengo yao ya kuona Simba kuendelea kuwa tishio ndani na nje ya Afrika.

Alisema mchakato wa uchaguzi ulikuwa mkubwa na kuwataka wanachama na mashabiki kuvunja makundi yaliyoundwa wa kipindi ambacho walikuwa kwenye kampeni ya uchaguzi na sasa kusimama pamoja.

"Mchakato ulikuja na kila mwanachama wa Simba ametumia vizuri demokrasia yake ya kuchagua anayemtaka, sasa tumeshapata uongozi mpya na tunatakiwa kuvunja makundi yetu yote na kushikamana na wale waliokuwa upande wangu marufuku kuwabeza walioshindwa, kwa sababu wote tunalengo moja," alisema Mangungu.

Aliongeza; "Ninaahidi kushirikiana kimawazo na wale ambao walikuwapo katika kinyang'anyiro cha uchaguzi hasa katika yale maneno yao ya kuitaka Simba kuwa imara kwa kuyatekeleza kwa vitendo.

"Sisi viongozi tulioingia madarakani tunatakiwa kuwa pamoja na kwa uhakika kabisa nitakuwa tayari kutumia mawazo na mpinzani wangu Kaluwa katika kuhakikisha Simba inasonga mbele."

Kwa upande wake Kaluwa alisema kwamba, "Sina mashaka na matokeo haya nimeyapokea kiroho safi, niwaombe wale wote waliokuwa upande wangu kuvunja yale makundi na sasa tuungane na uongozi huu mpya kufanikisha malengo tunayotarajia ndani ya klabu yetu kwa mpira uchezwe na kupata furaha."

Mangungu pia alipata na safu yake ya wajumbe watano wa Bodi ya Wakurugenzi.

Wajumbe hao ni Dk. Seif Muba amepata kura 1,636, CPA Issa Masoud Iddi (1,285), Rodney Chiduo (1,267), Seleman Harubu ameshinda kwa kura 1,250 na Asha Baraka amepata kura 1,564 wametetea kiti chao baada ya kumalizika kwa muda wao na sasa wanaendelea hadi 2027.

**TFF YAPONGEZA**

Wakati huo huo, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kupitia kwa Rais wake, Wallace Karia, limempongeza Mangungu kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, pamoja na Bodi ya Wakurugenzi.

Taarifa iliyotolewa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, imesema Rais Karia amepongeza kuchaguliwa kwa Mangungu katika kipindi kingine kuiongoza klabu hiyo, inao-


INAENDELEA UKURASA 23


## Rais wa Yanga atoa neno kuhusu Fei Toto

**Na Hadija Mngwai**

RAIS wa Yanga, Heris Said, amewatoa hofu mashabiki wa klabu hiyo juu ya mchezaji wao Feisal Salum ' Fei Toto' kwa kusema kuwa atarudi kikosini wakati sahihi utakapofika.

Mwaka jana Fei Toto aliingia katika mgogoro na klabu yake ya Yanga kufuatia kutaka kuvunja mkataba kinyume na sheria jambo ambalo uongozi huo ulilipinga na kudai bado ina mkataba na nyota huyo hadi mwaka 2024.

Aidha, suala hilo likifikishwa katika kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ambayo iliamua kuwa mchezaji huyo ni mali halali ya Yanga, lakini hadi sasa nyota huyo hajajiunga na kikosi chake.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Heris amesema kuwa, Feisal atarudi tu klabuni hapo kilichokuwapo sasa ni suala la wakati tu.

"Feisal ni mchezaji halali wa Yanga, hatuna sababu ya kuzungumza mengi kama watu walivyokuwa na mashaka na


INAENDELEA UKURASA 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >